**JAMHURI YA KENYA**

**WIZARA YA ELIMU**

# MTAALA WA SHULE YA JUNIA

# KISWAHILI

# GREDI YA 9

# KWA WANAFUNZI WALIO NA CHANGAMOTO ZA KUONA

**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

***JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI***

Toleo la Kwanza 2023

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN: 978-9914-43-434-7**

Umechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

**UTANGULIZI**

Serikali ya Kenya inajitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera kuhusu elimu, mafunzo, na utafiti yanakidhi matarajio ya Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya Kenya 2030, Sera ya Mtaala wa Kitaifa ya 2019, Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Kenya imesaini. Kuelekea kufikia lengo la Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu (MoE) imetekeleza kwa mafanikio na hatua kwa hatua utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi (CBC) katika ngazi ya awali, Shule ya msingi na Shule ya Junia.

Utekelezaji wa Mtaala wa Kitaalamu unajumuisha ufuatiliaji na tathmini ili kubaini mafanikio yake. Baada ya mzunguko wa miaka mitano wa utekelezaji, tathmini ya jumla ya mzunguko wa elimu ya msingi ilifanywa ili kubaini kufikia malengo ya matokeo ya kujifunza kama ilivyotarajiwa katika Mfumo wa Mtaala wa Elimu ya Msingi.

Serikali ya Kenya iliunda Jopo Kazi la Rais kuhusu Mageuzi ya Elimu'Presidential working party on Education Reforms' (PWPER) mwaka 2022 kushughulikia masuala muhimu yanayoathiri sekta ya elimu. PWPER ilifanya mapendekezo ya mbalimbali, yaliyochangia marekebisho ya mtaala. Mapendekezo ya PWPER, ripoti za ufuatiliaji, tathmini ya jumla, maoni kutoka kwa watekelezaji wa mtaala, na wadau wengine, yalisababisha hatua ya kufanya marekebisho katika mtaala pamoja na kuchunguza upya masomo yaliyopendekezwa.

Mtaala wa Gredi ya **9** kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona uliofanyiwa marekebisho, umejengwa kutokana na umilisi uliokuzwa katika gredi ya **Nane**. Umuhimu katika gredi hii ni maendeleo ya usomaji wa msingi, hesabu, na stadi za mwingiliano na mazingira.

Mitaala hii inawakilisha Malengo ya Kitaifa ya Elimu, kauli kiini, matokeo yanayotarajiwa kwa ujumla na kwa kila somo pamoja na Mada na Mada Ndogo. Mitaala hiyo pia inajuimuisha Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa, Swali Dadisi Lililopendekezwa, Umilisi wa kimsingi unaokuzwa, masuala mtambuko (PCI's), maadili, vigezo na viwango vya kuzingatia katika kutathmini.

Nina matumaini kwamba mashirika yote ya serikali na wadau wengine katika Elimu watatumia miundo hii kubuni ufanisi na ufanisi utekelezaji wa CBC.

**MHE. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU**,
**WIZARA YA ELIMU**

## DIBAJI

Wizara ya Elimu (MoE) ilianza kutekeleza Mtaala wa Kiumilisi (CBC) mwaka 2019 nchini kote. Gredi ya **7** ndiyo ya kwanza katika ngazi ya Elimu ya Shule ya Junia nayo Gredi ya **9** ni ya mwisho katika ngazi hiyo katika mfumo uliofanyiwa marekebisho wa elimu.

Mtaala uliofanyiwa marekebisho wa Gredi **ya 9** unaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi kutoka Gredi ya **8**. Mtaala huu unatoa fursa kwa wanafunzi kuzingatia wanachokipenda ili kuunda msingi wa elimu na mafunzo zaidi na/au kupata stadi za ajira. Kiwango hiki cha elimu ni muhimu sana katika kuchangia kufikia ruwaza na mwito wa marekebisho yanayoendelea ya kimtaala kama ilivyoelekezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 kuhusu Kuelekea kuafikia elimu na mafunzo yenye ubora, faafu na jumuishi kwa maendeleo endelevu nchini Kenya ''*Towards Realizing Quality, Relevant and Inclusive Education and Training for Sustainable Development'*. Mswada Elekezi huo unaeleza kuhusu kuvuka kutoka mtaala wa Kimafunzo na kuzingatia kukuza vipawa vya kila mwanafunzi.
Hivyo basi, Mtaala wa Gredi ya **9** kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona inalenga kuimarisha ukuzaji wa Umilisi wa Kimsingi katika mtaala huu, yaani: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu, uraia, ujuzi wa kidijitali, hamu ya kuendelea kujifunza na kujiamini.
Mitaala inapendekeza shughuli shirikishi za ujifunzaji unaolingana na Mada Ndogo mbalimbali na vipengele vingine vya mtaala wa umilisi (CBC). Pia inapendekeza baadhi ya nyenzo za kufundishia na mbinu za kutathmini mbalimbali. Inatarajiwa kwamba mitaala hii itaongoza walimu kufanikisha wanafunzi kufikia matokeo maalum yanayotarajiwa ya kujifunza katika Gredi ya **9** na kuwaandaa kwa mpito laini kwa Gredi ya **10**. Zaidi ya hayo, ni matumaini yangu kuwa mwalimu atatumia mitaala iliyorekebishwa kufanya ujifunzaji uwe wa kuvutia, unaochangamsha na wa kufurahiwa.

**DKT. BELIO KIPSANG', CBS**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

## SHUKRANI

Sheria Nambari 4 ya 2013 (iliyorekebishwa 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) inaipa mamlaka Taasisi kukuza mitaala na nyenzo za utekelezaji mtaala kwa elimu ya msingi na taasisi za elimu na mafunzo. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote cha elimu huhusisha utafiti wa kina, ulinganishi wa kimataifa na uhusishaji mkubwa wa wadau. Kupitia kwa mchakato uliopangwa kikamilifu na wa mashauriano, KICD ilibuni Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) ambao unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

KICD hupata ufadhili kutoka kwa Serikali ya Kenya ili kuwezesha ufikiaji kikamilifu wa majukumu na utekelezaji wa mipango ya serikali na sekta za Wizara ya Elimu. Taasisi pia inapata msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo unaolenga miradi mahususi. Mtaala wa Gredi ya 9 kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona umeandaliwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mpango wa *Kenya Secondary Education Quality Improvement Programme (SEQIP)* ulio chini ya uelekezi wa Wizara ya Elimu. Kwa hivyo, Taasisi inatoa shukrani za dhati kwa msaada kutoka kwa Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Elimu na washirika wengine wa maendeleo kwa sera na msaada wa mali na mikakati. Taasisi inatoa shukrani za kipekee kwa Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu katika Idara ya Serikali ya Mafunzo ya Awali na Elimu ya Msingi.

Tungependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wakufunzi walioshiriki kama wanajopo katika ukuzaji wa mitaala. Nashukuru pia Mashirika Huru ya Serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali kwa michango yao katika kuuandaa Mtaala wa Gredi ya 8 kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona. Kwa mintarafu hii, tunatambua msaada wa Afisa Mkuu Mtendaji wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza la Kitaifa la Mitihani nchini Kenya (KNEC) kwa usaidizi wao katika mchakato mzima wa kuuandaa mtaala.

Mwisho, tunamshukuru Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) na wanachama wengine wa Baraza kwa uelekezi wao wa mara kwa mara katika mchakato huu. Tunawahakikishia walimu wote, wazazi na wadau wengine kuwa mtaala huu utaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya 9 na uandaaji wa wanafunzi walio na changamoto za kuona kwa Daraja ya Juu Shule za Upili.

**PROF. CHARLES O. ONG'ONDO, PhD, MBS**
**MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI MKUU**
**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

**YALIYOMO**

UTANGULIZI ..... ii
DIBAJI ..... iii
SHUKRANI ..... iv
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ..... vi
MGAO WA VIPINDI ..... viii
KAULI KIINI ..... x
MATOKEO YA KUJIFUNZA KWA UJUMLA ..... xi
1.0 USAFI WA MAZINGIRA ..... 1
2.0 MAZOEZI YA VIUNGO VYA MWILI ..... 10
3.0 UTUNZAJI WA WANYAMA ..... 18
4.0 UTUNZAJI WA MALIASILI ..... 26
6.0 USALAMA BARABARANI ..... 43
7.0 HUDUMA KATIKA ASASI ZA KIJAMII ..... 52
8.0 MISUKOSUKO YA KIJAMII ..... 61
9.0 MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA BIASHARA ..... 71
10.0 KUKABILIANA NA MSONGO WA MAWAZO ..... 79
11.0 HAKI ZA KIBINADAMU ..... 88
12.0 MAGONJWA YANAYOTOKANA NA MIENENDO YA MAISHA ..... 98
13.0 MSHIKAMANO WA KIJAMII ..... 107
14.0 MATUMIZI YA USHURU ..... 115
15.0 MAADILI YA KITAIFA ..... 123
VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINI ..... 131
KIAMBATISHO 1: MWONGOZO WA MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI KATIKA GREDI YA TISA ..... 139
KIAMBATISHO 2: MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI ..... 142

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

**1. Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**

Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana itakayowezesha jamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia uhai wa taifa.

**2. Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**

Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa nchi kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

a) **Mahitaji ya kijamii**

Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mapinduzi kimyakimya ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

b) **Mahitaji ya kiuchumi**

Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika na wa humu nchini.

c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**

Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwengu

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**

Elimu inapaswa kumwezesha mtu kutambua, kukuza na kuimarisha kipawa chake ili aweze kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
Usawa wa kijamii kwa mfano usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa. Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zilizo na changamoto kwa mazoezi ya pamoja na ushirika katika huduma za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
Elimu inafaa kutoa nafasi kwa wanaosoma kuelewa, kuthamini, kukuza na kudumisha tamaduni faafu na kudondoa zile potofu kulingana na jamii ya wakati uliopo ili kujenga jamii ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Elimu inafaa pia kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira. Inafaa kuwaelekeza vijana wa Kenya kukubali haja ya mazingira safi.

**MGAO WA VIPINDI**

| S/NO | LEARNING AREA | VIPINDI KWA WIKI (DAKIKA 41 KWA KIPINDI) |
|---|---|---|
| 1 | English for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 2 | Kiswahili for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 3 | Mathematics for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 4 | Religious Education | 4 |
| 5 | Social Studies for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 6 | Integrated Science for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 7 | Pre-Technical Studies for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 8 | Agriculture And Nutrition for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 9 | Creative Arts And Sports for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 10 | Pastoral/Religious Instruction Programme | 1 |
| | **Total** | 41 |

## MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA SHULE YA JUNIA

Kufikia mwisho wa elimu ya Shule ya Junia, mwanafunzi aweze:

1. kutumia ujuzi wa kusoma na kuandika, ujuzi wa kuhesabu na kufikiri kimantiki ifaavyo katika kujieleza,
2. kuwasiliana kikamilifu katika miktadha mbalimbali,
3. kudhihirisha ujuzi wa kijamii, pamoja na tunu za kiimani na kimaadili kwa ajili ya mahusiano mema,
4. kutalii, kubadilisha, kusimamia na kutunza mazingira ifaavyo kwa ajili ya ujifunzaji na maendeleo endelevu,
5. kufanya usafi, kufuata kanuni zifaazo za usafi na lishe ili kuimarisha afya
6. kudhihirisha mienendo ya kimaadili na kuonyesha uraia mwema kama wajibu wa kiraia,
7. kuonyesha ridhaa kwa mirathi mingi na tofauti ya kitamaduni nchini ili kuleta mshikamano wa kimahusiano,
8. kudhibiti masuala mtambuko katika jamii ifaavyo
9. kutumia ujuzi wa kidijitali ifaavyo kwa madhumuni ya mawasiliano na ujifunzaji.

## KAULI KIINI

Somo la Kiswahili litampa mwanafunzi wa Daraja ya Awali Shule za Upili umilisi katika shughuli za kila siku. Umilisi huu utajengea haiba na uwezo wake wa kuwasiliana na kuhusiana katika jamii, kitaifa na kimataifa. Aidha, litamwendeleza kielimu na kumwandaa kwa ulimwengu wa kazi. Somo hili litampa mwanafunzi hamasa ya kumudu na kufurahia lugha na fasihi kwa kuzihusisha na tajriba na mazingira yake. Hali kadhalika, litampa mwanafunzi maarifa ya kijamii na kitamaduni. Mwanafunzi ataweza kujieleza na vilevile kupata fursa ya kutoa huduma kwa jamii.

## MATOKEO YA KUJIFUNZA KWA UJUMLA

Kufikia mwisho wa Shule ya Junia, mwanafunzi aweze:

1. kujieleza ipasavyo kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa njia ya maandishi na mazungumzo,
2. kuwasiliana ipasavyo katika miktadha mbalimbali ya kijamii
3. kujenga desturi ya kusoma na kufasiri maandishi kwa ufasaha
4. kutumia lugha kiubunifu kusimulia na kuandika tungo mbalimbali
5. kushiriki katika shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji,
6. kutumia teknolojia ipasavyo katika ujifunzaji na mawasiliano ili kukuza ujuzi wa kidijitali,
7. kutumia maadili yanayohitajika maishani kupitia stadi za lugha ya Kiswahili,
8. kufurahia na kuthamini lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi, ya taifa na kimataifa.

**MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO**

| **MADA** | **MADA NDOGO** | **MUDA ULIOPENDEKEZWA** |
|---|---|---|
| **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | 1. Kusikiliza na Kujibu; Mjadala<br>2. Kusikiliza kwa Kina; sauti /b/ na /mb/<br>3. Semi; tashbihi, sitiari na methali<br>4. Semi; vitendawili na nahau<br>5. Ufahamu wa Kusikiliza<br>6. Kusikiliza kwa Kufasiri<br>7. Kusikiliza kwa Kutathmini<br>8. Uzungumzaji wa Kushawishi<br>9. Kusikiliza kwa Kina: sauti **/j/** na **/nj/**<br>10. Mazungumzo; Malumbano ya Utani<br>11. Uzungumzaji katika Sherehe<br>12. ufahamu wa Kusikiliza<br>13. Mazungumzo; Mawaidha<br>14. Mawaidha<br>15. Kusikiliza kwa Kutathmini | 2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2 |
| **KUSOMA** | 1. Kusoma kwa Ufahamu Simulizi<br>2. Kusoma kwa Mapana<br>3. Kusoma kwa Kina; Ushairi<br>4. Kusoma kwa Ufasaha<br>5. Kusoma kwa Ufahamu<br>6. Kusoma kwa Kina; Ushairi<br>7. Ufupisho<br>8. Kusoma kwa Kina; Ushairi<br>9. Ufahamu wa Kifungu cha Kushawishi<br>10. Kusoma kwa Kina; Ushairi | 2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 11. Kusoma kwa Mapana<br>12. Kusoma kwa Ufasaha<br>13. Kusoma kwa Kina; Ushairi<br>14. Kusoma kwa Ufahamu<br>15. Ufupisho | 2<br>2<br>2<br>2<br>2 |
| **KUANDIKA** | 1. Viakifishi; koloni na semi koloni<br>2. Insha za Kiuamilifu; Barua ya kirafiki<br>3. Insha za Kubuni; Masimulizi<br>4. Insha za Kubuni; Masimulizi<br>5. Insha za Kiuamilifu; Shajara<br>6. Insha za Kubuni; Methali<br>7. Insha za Kubuni; Maelezo<br>8. Viakifishi; mabano na kistari kifupi<br>9. Insha za Kubuni; Masimulizi<br>10. Insha za Kiuamilifu; Barua ya Kuomba Kazi<br>11. Insha za Kubuni; Maelezo<br>12. Insha za Kiuamilifu; Hotuba ya Kushawishi<br>13. Insha za Kubuni; Maelezo<br>14. Insha za Kiuamilifu; Shajara<br>15. Kujibu | 2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2 |
| **SARUFI** | 1. Vihusishi vya Mahali na Wakati<br>2. Vihusishi vya -a unganifu na vya sababu<br>3. Vihusishi Vilinganishi na Kihusishi na<br>4. Nyakati na Hali; -ki- ya masharti<br>5. Hali za Masharti; -nge- na - ngali-<br>6. Vielezi vya Namna na vya Wakati<br>7. Vielezi vya Mahali na vya Idadi | 2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2<br>2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 8. Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi- ngeli ya U-ZI naYA-YA, LI, KU na PA-KU-MU<br>9. Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi<br>10. Vinyume vya Vihusishi<br>11. Mnyambuliko wa Vitenzi; kauli ya kutendana, kutendeana na Kutendesha<br>12. Aina za Sentensi; sentensi tata<br>13. Ukanushaji; -nge- ,-ngali-, na -ki-<br>14. Udogo na Ukubwa wa Nomino<br>15. Usemi halisi na Usemi wa Taarifa | 2<br>2<br>2<br><br>2<br>2<br>2<br>2<br>2 |

## 1.0 USAFI WA MAZINGIRA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Kusikiliza na Kujibu**<br><br>Mjadala<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mjadala,<br>b) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kuchangia mjadala,<br>c) kushiriki mjadala kwa kuzingatia vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kuchangia mijadala,<br>d) kuchangamkia kushiriki katika mijadala ya miktadha mbalimbali. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mjadala akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika kuchangia mjadala akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza au atazame mjadala kuhusu suala lengwa katika kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza vipengele vya kusikiliza na kuchangia mjadala vilivyozingatiwa katika mjadala alioisikiliza.<br>● Mwanafunzi ashiriki mjadala kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake akizingatia vipengele vifaavyo vya mjadala. | Kwa nini ni umuhimu wa kusikiliza na kuchaangia mjadala? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaendeleza ujuzi wa kuzungumza na kuongea anapoongea na kupeana maoni yake kuhusu vipengele vifaavyo na kutetea hoja zake katika mjadala.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaonyesha ujuziwa utafiti mtandaoni anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile redio na kanda za sauti katika kusikiliza au kutazama mijadala mbalimbali.
- Ubunifu: mwanafunzi anaonyesha ufundi wa kiubunifu anapotumia mitindo anuwai kuwashawishi wenzake katika mjadala kuhusu suala lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anakuza ujasiri anapochangia kwa kutoa maoni katika mjadala ipasavyo.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapoheshimu zamu ya wengine katika mazungumzo.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika kusikiliza au kutazama mjadala.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala kuhusu suala lengwa kuwashawishi wenzake.
- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kwa umakini.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia dhana ya kusikiliza na kujibizana.
- Integrated Science na Agriculture & Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia usafi wa mazingira.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video), vitabu mbalimbali (vilivyo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza/zilizo na vyenye maandishi ya breli)

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Liliopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu Simulizi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha simulizi,<br>b) kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha simulizi,<br>c) kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha simulizi,<br>d) kueleza maana ya msamiati kama ulivyotumiwa katika kifungu cha simulizi,<br>e) kuchangamkia kujibu maswali ya ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua habari mahususi katika kifungu cha ufahamu cha simulizi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu cha simulizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha ufahamu cha simulizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutabiri matukio katika kifungu cha ufahamu simulizi chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza kutokana na picha au matukio. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutabiri matukio katika kifungu cha ufahamu simulizi chenye maandishi ya breli kutokana na maelezo ya picha au ya matukio.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kufasiri habari kutokana na kifungu cha ufahamu cha simulizi chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza akiwa mwenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kufasiri habari kutokana na kifungu cha ufahamu cha simulizi chenye maandishi ya breli akiwa mwenzake akiwa mwenzake. | Unadondoa vipi habari zilizo katika ufahamu wa simulizi kwa usahihi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya maneno au msamiati kulingana na matumizi yake kimuktadha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwatungia wenzake sentensi akitumia msamiati wa suala lengwa kwa usahihi ili azitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anakuza ujuzi wa kuzungumza anapochangia kikamilifu katika shughuli za kikundi kudondoa habari mahususi katika kifungu.
- Kujiamini: mwanafunzi anaendeleza ujuzi wa kujieleza anapoweza kutumia msamiati wa suala lengwa kutunga sentensi sahihi.
- Ubunifu: mwanafunzi anaonyesha ujuzi wa kiubunifu kwa kutunga sentensi sahihi akitumia msamiati wa suala lengwa.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapokubaliana na maoni ya wenzake na kushirikiana nao katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutunza kifaa cha kidijitali.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu kuhusu usafi wa mazingira.
- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa na kuzingatia ujumbe.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Language: masomo haya pia yanashughulikia kusoma ufahamu.
- Integrated Science na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia suala la usafi wa mazingira.

| |
|---|
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vyenye maandishi ya breli na vitabu vyenye hati zinazofaa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Viakifishi**<br><br>(Vipindi 2**)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya koloni na semi koloni katika matini<br>b) kueleza matumizi ya koloni na semi koloni katika matini<br>c) kutumia alama ya koloni na semi koloni katika matini (aliye na upungufu wa kuona),<br>d) kutumia nukta nundu zinazounda alama ya koloni na semi koloni ipasavyo katika matini, (asiyeona)<br>e) kufurahia matumizi yafaayo ya alama ya koloni na semi koloni katika matini mbalimbali. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua alama ya koloni na semi koloni katika maneno, sentensi au vifungu kwenye matini andishi au za kidijitali zenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nukta nundu zinazotumika kuunda alama ya koloni na semi koloni katika maneno, sentensi au vifungu kwenye matini andishi au za kidijitali zenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza matumizi ya koloni na semi koloni katika matini akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika maneno, sentensi au vifungu kwa kutumia alama ya koloni na semi koloni ipasavyo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika maneno, sentensi au vifungu kwa kutumia | 1. Je, alama ya koloni hutumiwa vipi katika maandishi?<br>2. Kwa nini ni muhimu kutumia alama ya semi koloni katika maandishi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | nukta nundu zinazounda alama ya koloni na semi koloni ipasavyo.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia alama ya koloni na semi koloni ipasavyo na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili wakitolee maoni. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia nukta nundu zinazounda alama ya koloni na semi koloni ipasavyo na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili wakitolee maoni.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ashirikiane na wenzake kusahihisha kifungu kuhusu suala lengwa ambacho hakijatumia alama ya koloni na semi koloni ipasavyo. Mwanafunzi asiyeona ashirikiane na wenzake kusahihisha kifungu kuhusu suala lengwa ambacho hakijatumia nukta nundu zinazounda alama ya koloni na semi koloni ipasavyo.<br>• Mwanafunzi awasomee wenzake kifungu alichokiandika ili watambue matumizi ya alama ya koloni na semi koloni.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona amweleze mzazi au mlezi wake kuhusu maneno, sentensi au vifungu alivyoandika | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vilivyo na matumizi mbalimbali ya alama za koloni na semi koloni. Mwanafunzi asiyeona amweleze mzazi au mlezi wake kuhusu maneno, sentensi au vifungu alivyoandika vilivyo na matumizi mbalimbali ya nukta nundu zinazounda alama za koloni na semi koloni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anakuza ushirikiano anaposhirikiana na wenzake katika kusahihisha vifungu walivyoandika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaendeleza ujuzi wa kupika chapa anapotumia vifaa vya kidijitali *vyenye teknolojia saidizi* kuandika kifungu na kukisambaza mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anaendeleza ujuzi wa kiubunifu anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya alama za koloni na semi koloni.

**Maadili**

- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi aikuze anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa na kwenda kumsomea mzazi/mlezi alichojifunza.
- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia uakifishaji.
- Integrated Science na Home Science: masomo haya pia yanashughulikia usafi wa mazingira.

| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia** |
| --- |
| Kielelezo cha viakifishi koloni na semi koloni, tarakilishi/kipakatalishi chenye teknolojia saidizi, nakala ya kifungu kilicho na alama za uakifishaji, mashine ya breli, kielelezo cha matumizi ya koloni na semi koloni. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Vihusishi vya Mahali** na **Wakati**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vihusishi vya mahali na vya wakati katika matini,<br>b) kutumia vihusishi vya mahali na vya wakati katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi yafaayo ya vihusishi vya mahali na vya wakati katika matini mbalimbali. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa vihusishi vya mahali na vya wakati kutoka kwa kapu maneno, mti maneno, chati, vitabu zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika na kuorodhesha vihusishi vya mahali na vya wakati kutoka kwa kapu maneno, mti maneno, chati, vitabu zilizo na maandishi ya breli au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vihusishi vya mahali na vya wakati katika sentensi au vifungu kwenye vitabu vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuvipigia mstari au kuvikolezea wino. Mwanafunzi asiyeona atambue vihusishi vya mahali na vya wakati katika sentensi au vifungu kwenye vitabu vyenye maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuviandika kwa italiki. | 1. Kwa nini ni muhimu kutambua vihusishi vya mahali?<br>2. Je, vihusishi vya wakati vinatumika vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vihusishi vya mahali na vya wakati. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anakuza umisi wa ushirikiano anaposhiririkiana na wenzake kutambua vihusishi husika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anakuza ujuzi wa utafiti anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua vihusishi vya mahali na wakati.
- Ubunifu: mwanafunzi anaendeleza ujuzi wa kiubunifu anapotunga sentensi sahihi akitumia vihusishi vya mahali na wakati.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaonyesha heshima anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapoandika sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia viwakilishi mbalimbali.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia vihusishi vya mahali na vya wakati.
- Integrated Science na Agriculture & Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia usafi wa mazingira.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

- Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi, rununu yenye teknolojia saidizi, projekta, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno, chati, nyenzo halisi, vitabu vyenye fonti zinazofaa/vyenye maandishi ya breli.

## 2.0 MAZOEZI YA VIUNGO VYA MWILI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutamka sauti /b/ na /mb/ ili kuzitofautisha kimatamshi,<br>b) kutamka vitanzandimi vyenye sauti /b/ na /mb/,<br>c) kuunda vitanzandimi vyepesi vyenye sauti /b/ na /mb/,<br>d) kuchangamkia matamshi bora ya sauti /b/ na /mb/ katika mazungumzo ya kawaida. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua sauti /b/ na /mb/ katika maneno na vifungu vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua sauti /b/ na /mb/ katika maneno na vifungu zilizo na maandishi ya breli.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza na kutamka vitanzandimi vyepesi vinavyohusisha matamshi ya sauti /b/ na /mb/ katika kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kama vile simu, redio.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kubuni vitanzandimi vyepesi vinavyohusisha sauti /b/ na /mb/.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake vitanzandimi alivyovibuni ili wamtolee maoni. | Sauti **/b/** na **/mb/** hutofautianaje kimatamshi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anakuza ujuzi wa kutafiti anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kusikiliza vitanza ndimi vyenye sauti lengwa.
- Ubunifu: mwanafunzi anaonyesha ufundi wa kiubunifu anapotunga vitanzandimi vyepesi akitumia maneno yenye sauti lengwa.

| |
|---|
| ● Kujiamini: mwanafunzi anapotamka kwa ujasiri vitanzandimi ipasavyo yenye sauti lengwa.<br>● Hamu ya ujifunzaji mwanafunzi: mwanafunzi anapowasomea wenzake vitanzandimi alivyovibuni kwa kuhusisha matamshi bora ya sauti lengwa. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutunza kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi anachotumia.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Afya ya mtu binafsi: mawanafunzi anapobuni vitanzandimi akizingatia suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia dhana ya kutamka sauti.<br>● Creative Arts and Sports: somo hili pia linashughulikia mazoezi ya viungo vya mwili.<br>● Agriculture and Nutrition: somo hili pia linashughulikia masuala ya afya. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Chati, michoro na picha, mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video), vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia,<br>b) kutumia msamiati unaotokana na matini aliyosoma,<br>c) kufafanua ujumbe wa matini aliyosoma,<br>d) kujenga mazoea ya kusoma matini mbalimbali za kujichagulia. | ● Mwanaunzi aelekezwe kuteua matini kuhusu suala linalomvutia.<br>● Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma matini yenye maandishi ya breli aliyojichagulia na kutambua vipengele vyake muhimu. Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma matini yenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza aliyojichagulia na kutambua vipengele vyake muhimu.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua msamiati uliotumiwa katika matini aliyojichagulia kwa kutumia kamusi yenye fonti inayofaa kutafuta maana za maneno asiyoyajua. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua msamiati uliotumiwa katika matini aliyojichagulia kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kutafuta maana za maneno asiyoyajua.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutungia mwenzake sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufafanua ujumbe wa matini aliyosoma kwa ufupi. | 1. Unawezaje kujichagulia matini ya kusoma?<br>2. Kwa nini ni muhimu kusoma matini ya kujichagulia? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kusakura mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kujichagulia matini ya kusoma kisha afafanue maana ya msamiati na ujumbe katika matini hiyo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na mwenzake katika kikundi kutambua vipengele muhimu kuhusu suala lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi kutokana na msamiati wa matini ya kujichagulia.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia msamiati aliojifunza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kujichagulia matini ya kusoma.

**Maadili**.

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafuta na kusoma matini.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza.

**Masuala Mtambuko**
Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma matini ya kujichagulia kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa mapana.
- Creative Arts and Sports: somo hili pia linashughulikia mazoezi ya viungo vya mwili.
- Agriculture and Nutrition: somo hili pia linashughulikia masuala ya afya.

| **Mapendekezo ya nyenzo za kufundishia**<br>Kamusi yenye fonti inayofaa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. |
|---|

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Insha za Kiuamilifu**<br><br>Barua ya Kirafiki<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaoafiki katika kujibu barua ya kirafiki,<br>b) kueleza lugha inayofaa katika kujibu barua ya kirafiki,<br>c) kufafanua muundo unaofaa katika kujibu barua ya kirafiki,<br>d) kuandika barua ya kirafiki akizingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao, (aliye na upungufu wa kuona)<br>e) kuandika barua ya kirafiki akizingatia ujumbe, lugha, muundo, sheria za matumizi ya mikato, alama za uakifishaji na herufi kubwa za breli(asiyeona),<br>f) kujenga mazoea ya kujibu barua ya kirafiki katika maisha ya kila siku. | • Mwanafunzi aelekezwe kutambua ujumbe unaoafiki anapojibu barua ya kirafiki kwa kujadiliana na mwenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kueleza lugha inayofaa kujibu barua ya kirafiki akishirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujadili muundo wa barua ya kirafiki akishirikiana na wenzake katika kikundi<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika barua ya kirafiki ya kumjibu rafiki yake, akizingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao. Mwanafunzi asiyeona aandike barua ya kirafiki ya kumjibu rafiki yake, akizingatia ujumbe, lugha, muundo, sheria za matumizi ya mikato, alama za uakifishaji na herufi kubwa za breli. | Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele unapojibu barua ya kirafiki? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi amsomee wenzake barua aliyoiandika ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili vipengele vya kujibu barua ya kirafiki.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika barua ya kuijibu barua ya kirafiki.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake barua aliyoandika.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapoandika barua kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Language: masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa barua ya kirafiki.
- Creative Arts and Sports: somo hili pia linashughulikia mazoezi ya viungo vya mwili.
- Agriculture and Nutrition: somo hili pia linashughulikia masuala ya afya.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Kielelezo cha barua ya kirafiki, vifaa vya kuandikia breli, vitabu vya ziada vyenye hati zinazofaa/vyenye maandishi ya breli.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Vihusishi vya -a Unganifu** na **vya Sababu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vihusishi vya a- unganifu na vya sababu katika matini,<br>b) kutumia vihusishi vya a- unganifu na vya sababu ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi yafaayo ya vihusishi vya a- unganifu na vya sababu katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vihusishi vya **a-** unganifu na vya sababu kutoka kwa kapu maneno, mti maneno, chati zilizo na fonti zifaazo na zisizotatiza au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi aelekezwe kutambua vihusishi vya **a-** unganifu na vya sababu kutoka kwa kapu maneno, mti maneno, chati zilizo na maandishi ya breli au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vihusishi vya a-unganifu na vya sababu katika sentensi au vifungu kwenye vitabu vyenye fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vihusishi vya a- unganifu na vya sababu katika sentensi au vifungu kwenye vitabu vyenye maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vihusishi vya a- unganifu na vya sababu akishirikiana na wenzake. | Ni vipi unatofautisha vihusishi vya A-Unganifu na vya Sababu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake sentensi zinazotumia vihusishi vya a- unganifu na vya sababu. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua vihusishi vya -a unganifu na vya sababu.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vihusishi vya -a unganifu na vya sababu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake vihusishi vya a- unganifu na vya sababu katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapotunga sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Language: masomo haya pia yanashughulikia vihusishi.
- Integrated Science na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya afya.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Tarakilishi/vipakatalishi *vyenye teknolojia saidizi*, rununu *yenye teknolojia saidizi*, projekta, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno, michoro, chati, vifaa halisi

### 3.0 UTUNZAJI WA WANYAMA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Semi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya tashbihi, sitiari na methali ili kuzipambanua.<br>b) kutambua tashbihi, sitiari na methali katika matini ya fasihi simulizi,<br>c) kueleza matumizi ya tashbihi, sitiari na methali katika matini ya fasihi simulizi,<br>d) kutumia tashbihi, sitiari na methali katika uwasilishaji wa tungo za fasihi simulizi,<br>e) kuchangamkia matumizi ya tashbihi, sitiari na methali katika tungo za fasihi simulizi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya tashbihi, sitiari na methali akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua tashbihi, sitiari na methali kutoka kwenye tungo simulizi, kapu la semi, au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua tashbihi, sitiari na methali kutoka kwenye tungo simulizi, orodha ya semi, au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusakura matumizi ya tashbihi, sitiari na methali katika tungo za fasihi simulizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na mwenzake matumizi ya tashbihi, sitiari na methali alizozitafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushiriki katika uwasilishaji wa tashbihi, sitiari na methali akishirikiana na wenzake katika kikundi. | 1. Tunatumia mbinu za lugha katika kuwasilisha tungo za fasihi simulizi kivipi?<br>2. Kwa nini tunatumia tashbihi, sitiari na methali kuwasilisha tungo za fasihi simulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na wenzake kujadili ujumbe na lugha katika tashbihi, sitiari na methali.<br>● Mwanafunzi amwelezee mzazi au mlezi wake kuhusu tashbihi, sitiari na methali katika jamii yake ili amtolee maoni yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili maana za tashbihi, sitiari na methali.
- Ubunifu: mwanafunzi anapowasilisha tashbihi, sitiari na methali kwa mitindo anuwai.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwelezea mzazi wake kuhusu tashbihi, sitiari na methali katika jamii yake.
- Uraia: mwanafunzi anapojifunza kuhusu tashbihi, sitiari na methali za jamii yake na kuthamini.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kusikiliza tashbihi, sitiari na methali na kuzichanganua.

**Maadili**

- Uzalendo: mwanafunzi anapoelezea tashbihi, sitiari na methali za jamii yake na kuzionea fahari.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia darasani.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya utunzaji wa wanyama : mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kutambua tashbihi, sitiari na methali kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapowazia kuhusu umuhimu wa wanyama.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia tungo za fasihi simulizi.

| |
|---|
| Agriculture and Nutrition: somo hili pia linashughulikia masuala ya utunzaji wa wanyama. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>● Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video), vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli. |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>Ushairi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya shairi ili kulitofautisha na tungo nyingine,<br>b) kufafanua sifa za ushairi kama utanzu wa fasihi andishi,<br>c) kueleza sifa za ushairi katika shairi,<br>d) kufurahia kuchambua ushairi kama utungo wa fasihi. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutafiti maana ya shairi vitabuni vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au mtandaoni kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi ili kulitofautisha na tungo nyingine akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutafiti maana ya shairi vitabuni vyenye maandishi ya breli au mtandaoni kwa kutumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi ili kulitofautisha na tungo nyingine akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili sifa za ushairi kama utanzu wa fasihi andishi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, magazetini au vitabuni vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza na | 1. Kwa nini shairi ni tofauti na tungo zingine?<br>2. Utasoma shairi kivipi ili kuvutiwa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kueleza sifa za ushairi katika mashairi hayo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutafiti mtandaoni kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi au vitabuni vyenye maandishi ya breli na kueleza sifa za ushairi katika mashairi hayo.<br>● Mwanafunzi awasome wenzake sifa alizotambua katika mashairi aliyoyasoma ili wamtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposoma shairi akiwa na wenzake katika kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake sifa za shairi alilosoma.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni shairi na kuchambua sifa zake kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposoma shairi na kuchambua sifa zake.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anaposoma shairi, mtazamo wake wa uonoulimwengu unaweza kubadilika na kukua.

| |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia usomaji wa kina.<br>● Social Studies na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia utunzaji wa wanyama. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya marejeleo vya breli vitabu vya marejeleo yenye hati inayofaa |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>Masimulizi<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kufafanulia ujumbe wa insha ya masimulizi,<br>b) kufafanua ujumbe wa insha ya masimulizi kupitia kwa utangulizi,<br>c) kufafanua ujumbe wa insha ya masimulizi kupitia kwa wahusika,<br>d) kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia ujumbe na muundo ufaao,<br>e) kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia ujumbe, muundo ufaao, sheria za matumizi ya mikato, alama za | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kufafanulia ujumbe wa simulizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufafanua ujumbe wa insha ya masimulizi kupitia kwa utangulizi kutoka kwa kielelezo cha insha ya masimulizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kielelezo cha insha ya masimulizi kuhusu suala lengwa atakachopewa na mwalimu au atakachosoma kwenye matini za aina mbalimbali na kujadili na wenzake kuhusu ufafanuzi wa ujumbe kupitia kwa utangulizi na mazungumzo ya wahusika.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya masimulizi | Utasimulia vipi jambo ili ujumbe wako upate kueleweka zaidi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | uakifishaji na herufi kubwa za breli(asiyeona),<br>f) kufurahia kufafanua ujumbe wa insha ya kusimulia ili kufanikisha maelezo. | akizingatia ufafanuzi ufaao wa ujumbe, kupitia kwa wahusika. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya masimulizi akizingatia sheria za matumizi ya mikato, alama za uakifishaji na herufi kubwa za breli na ufafanuzi ufaao wa ujumbe kupitia kwa wahusika.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwasomea wenzake insha aliyoandika darasani au kuwasambazia kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi ili waitolee maoni.<br>● Mwanafunzi ashirikiana na wenzake kusahihisha insha ya masimulizi aliyoandika kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia ufafanuzi ufaao wa ujumbe. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusahihisha insha ya masimulizi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusambazia insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi akizingatia ufafanuzi ufaao wa ujumbe kupitia kwa wahusika.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha na kuwasomea wenzake.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapoandika insha ya kubuni kuhusu suala lengwa.

| **Uhusiano na Masomo Mengine** |
| --- |
| ● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia stadi ya kuandika.<br>● Social Studies na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia utunzaji wa wanyama. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya masimulizi, tarakilishi/kipakatalishi, nakala ya kifungu cha insha ya masimulizi, vitabu vyenye fonti zifaazo/vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Kihusishi na** na **Vihusishi Vilinganishi**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika matini.<br>b) kutumia kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi ipasavyo katika matini.<br>c) kuchangamkia kutumia kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika kapu maneno, mti maneno, chati, orodha ya maneno zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika na kuorodhesha kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika kapu maneno, mti maneno, chati, orodha ya maneno zilizo na maandishi ya breli au katika tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika sentensi au vifungu kwenye vitabu vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe | Utatumiaje vihusishi vilinganishi unavyovijua? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutambua kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika sentensi au vifungu kwenye vitabu vyenye maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi amtajie mzazi au mlezi wake kihusishi **na** na vihusishi vilinganishi katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili aina za vihusishi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua kihusishi na na vihusishi vilinganishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua kihusishi na na vihusishi vilinganishi katika matini na kuvitungia sentensi sahihi na vifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake kihusishi na na vihusishi vilinganishi katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapoandika sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa.

| **Uhusiano na Masomo Mengine** |
| --- |
| ● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia vihusishi.<br>● Integrated Science na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya afya. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno michoro, chati/kadi za breli, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa, vifaa vya kuandikia breli. |

## 4.0 UTUNZAJI WA MALIASILI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Semi**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vitendawili na nahau ili kuipambanua,<br>b) kutambua vitendawili na nahau katika matini ya fasihi simulizi,<br>c) kufafanua umuhimu wa vitendawili na nahau katika fasihi simulizi,<br>d) kutumia nahau ipasavyo katika mawasiliano,<br>e) kuwasilisha vitendawili kwa kuzingatia vipengele vya uwasilishaji wake,<br>f) kuchangamkia matumizi ya nahau na uwasilishaji wa | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya vitendawili akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya nahau akishirikiana na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi au maktabani umuhimu wa vitendawili na nahau.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua nahau mbalimbali katika matini andishi au ya kidijitali ya fasihi simulizi na kueleza maana zake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa | 1. Kwa nini vitendawili ni muhimu?<br>2. Unawasilisha vitendawili kivipi?<br>3. Kwa nini tunatumia nahau katika mawasiliana? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | vitendawili katika tungo za fasihi. | kutumia nahau mwafaka. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika sentensi upya katika breli na kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia nahau mwafaka.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia nahau ipasavyo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya uwasilishaji wa vitendawili akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aaelekezwe kusikiliza vitendawili katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au kutoka kwa mwalimu na kubainisha vipengele vya kimsingi vya uwasilishaji wa vitendawili.<br>● Mwanafunzi awawasilishie wenzake vitendawili kwa kuzingatia vipengele vya uwasilishaji wa vitendawili.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na mzazi au mlezi wake kutambua vitendawili na nahau katika jamii yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kuwasilisha vitendawili na nahau katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kuwasilisha vitendawili na nahau katika kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotega na kutegua vitendawili, anapotoa maana za nahau na kuchangia katika kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutambua vitendawili na nahau kutoka kwa jamii yake.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika majadiliano ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika kuwasilisha vitendawili na nahau katika kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi anaposhiriki katika kutega na kutegua vitendawili na wenzake kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposhiriki katika kutega na kutegua vitendawili na wenzake kuhusu suala lengwa.<br>● Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanawezesha kupunguza umaskini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia dhana ya tungo za fasihi simulizi.<br>● Social Studies: somo hili pia hushughulikia utunzaji wa maliasili. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Chati, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, vitabu mbalimbali vyenye hati zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli). |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha,<br>b) kusoma kifungu cha nathari akizingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu cha nathari akizingatia kasi ifaayo,<br>d) kusoma kifungu cha nathari akizingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>e) kusoma kifungu cha nathari akizingatia ishara za mwili zifaazo,<br>f) kujenga mazoea ya kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha nathari akizingatia matamshi bora.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu cha nathari chenye fonti inayofaana rangi isiyotatiza akizingatia kasi afaayo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu cha nathari chenye maandishi ya breli akizingatia kasi ifaayo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu cha nathari akizingatia kiwango kifaacho cha sauti.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu cha nathari akizingatia ishara za mwili zifaazo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu cha nathari akizingatia kiimbo au toni inayofaa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusakura kifungu cha nathari mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuwasomea wenzake kwa ufasaha.<br>● Mwanafunzi amsome mzazi au mlezi wake kifungu cha nathari kwa ufasaha ili akitolee maoni. | Utatambua vipi vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutambua na kujadili vipengele vya usomaji wa ufahamu.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya usomaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusakura kifungu cha nathari.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu wenzake wakisoma kifungu.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusoma kwa ufasaha.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala la maliasili katika mazingira yake.
- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.
- Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanawezesha kupunguza umaskini.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa ufasaha.
- Social Studies: somo hili pia hushughulikia dhana ya utunzaji wa maliasili.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya marejeleo vya breli kifungu cha nathari chenye hati inayofaa, kifungu cha nathari yenye maandishi ya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>Masimulizi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari ili kuibanisha,<br>b) kufafanua lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari katika insha ya masimulizi,<br>c) kuandika insha ya masimulizi akizingatia lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari,<br>d) kuandika insha ya masimulizi akizingatia lugha ya kitamathali, matumizi ya mikato ya breli, alama za uakifishaji breli, herufi kubwa za breli, matendo ya wahusika na mandhari(asiyeona),<br>e) kufurahia kuandika insha za masimulizi akizingatia lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari ufaao ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari katika masimulizi kwenye matini andishi au za kidijitali zenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aeelekezwe kusoma vielelezo vya insha ya kubuni kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali zenye teknolojia saidizi na kushirikiana na wenzake kubainisha lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya masimulizi kuhusu suala lengwa akitumia vipengele vifaavyo vya lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari ili kujenga taswira zifaazo<br>Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya masimulizi kuhusu suala lengwa akitumia vipengele vifaavyo vya lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari ili kujenga taswira zifaazo, akizingatia matumizi ya mikato, alama za uakifishaji na herufi kubwa za breli.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kusahihisha insha aliyobuni. | Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele unapoandika insha ya masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika kuhusu suala lengwa ili wachanganue lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na mandhari. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kuchanganua lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari katika insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha kwa kuzingatia lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari ufaao.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika na kuwataka wachanganue lugha ya kitamathali, matendo ya wahusika na uchoraji wa mandhari.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha aliyoandika.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.
- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.
- Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanawezesha kupunguza umaskini.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia vipengele vya masimulizi.

| |
|---|
| ● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya utunzaji wa maliasili. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/kipakatalishi, nakala ya insha ya kubuni, vifaa vya kuandikia breli, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4 .4 Sarufi** | **4.4.1 Nyakati na Hali**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua **-ki-** ya masharti katika matini,<br>b) kutumia **-ki-** ya masharti ipasavyo katika matini,<br>c) kutambua **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo katika matini,<br>d) kutumia **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo ipasavyo katika matini,<br>e) kujenga mazoea ya kutumia ipasavyo **-ki-** ya masharti na **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua **-ki-** ya masharti katika matini andishi au ya kidijitali akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-ki-** kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, chati yenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-ki-** kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu vyenye maandishi ya breli, kadi za breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kwa kuziandika kwa italiki akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kuonyesha matumizi ya hali ya **-ki-** akishirikiana na wenzake katika kikundi. | 1. **-ki-** ya masharti hutumika vipi katika sentensi?<br>2. **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo hutumiwa vipi katika sentensi?<br>3. Mbona unatumia **-ki-** ya masharti? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo katika sentensi mbalimbali akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza, tarakilishi  yenye teknolojia saidizi , kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona achague sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-ka-** ya kufuatana kwa vitendo kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kuonyesha matumizi ya hali ya -**ka**- ya kufuatana kwa vitendo akishirikiana na wenzake katika kikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua hali ya masharti -ki- na hali ya kufuatana kwa vitendo -ka-.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kwa kutumia hali ya masharti -ki- na kufuatana kwa vitendo -ka-.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua hali ya masharti –**ki-** na kufuatana kwa vitendo **-ka-** kisha kuzitungia sentensi sahihi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapodhamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.

| |
|---|
| ● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya mazingira na tabia ya nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.<br>● Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanawezesha kupunguza umaskini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English, Indigenous Languages na Foreign Languages: masomo haya pia yanashughulikia nyakati na hali mbalimbali.<br>● Social Studies na Agriculture: masomo haya pia yanashughulikia utunzaji wa maliasili. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, chati/kadi za breli, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa. |

| 5.0 MITAZAMO HASI YA KIJINSIA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza** (Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ufahamu wa kusikiliza,<br>b) kufafanua kanuni za ufahamu wa kusikiliza,<br>c) kueleza vipengele vya ufahamu wa kusikiliza,<br>d) kushiriki katika ufahamu wa kusikiliza akizingatia vipengele vyake,<br>e) kuchangamkia kushiriki katika kusikiliza kwa ufahamu ili kukuza stadi ya kusikiliza. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya ufahamu wa kusikiliza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili kanuni za ufahamu wa kusikiliza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya ufahamu wa kusikiliza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu au mgeni mwalikwa na kujibu maswali.<br>● Mwanafunzi asikilize matini kuhusu suala lengwa katika chombo cha kidijitali chenye teknolojia sidizi na kujibu maswali. | 1. Utapataje ujumbe unaposikiliza ufahamu wa kusikiliza?<br>2. Je, kwa nini ni muhimu kusikiliza ufahamu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza ujumbe aliopata kutokana na ufahamu wa kusikiliza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki shughuli ya kusikiliza kwa ufahamu ili kupata ujumbe.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza matini ya ufahamu.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposikiliza na kufasiri ujumbe ifaavyo.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofasiri ujumbe kutokana na ufahamu wa kusikiliza.

| |
|---|
| ● Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kusikiliza ufahamu na kujibu ipasavyo. |
| **Maadili**<br>● Uadilifu: mwanafunzi anapowasikiliza wasemaji kwa makini.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kufasiri ujumbe katika kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anaposikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusikiliza kwa ufahamu.<br>● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video), vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli). |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu cha ufahamu chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza na kudondoa | 1. Kwa nini tunasoma ufahamu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (Vipindi 2) | a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu,<br>b) kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha ufahamu,<br>c) kueleza maana ya msamiati kulingana na kifungu cha ufahamu,<br>d) kuchangamkia kusoma kwa ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | habari mahususi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu cha ufahamu chenye maandishi ya breli na kudondoa habari mahususi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza habari za kifungu cha ufahamu kwa ufupi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha ufahamu.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa msamiati wa suala lengwa kwenye kapu maneno, mti maneno, chati au kwenye vitabu zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika msamiati lengwa kutoka kwa matini yenye maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya msamiati kulingana na muktadha wa matumizi katika matini akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia maneno hayo kutunga sentensi sahihi kisha kumsomea mwenzake ili amtolee maoni. | 2. Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele tunaposoma ufahamu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma ufahamu akiwa na wenzake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia msamiati wa suala lengwa katika muktadha maalum.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Masuala ya jinsia: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia usomaji wa ufahamu.<br>● Religious Education na Social Studies: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya kijinsia. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, kapu maneno, kadi za breli, mti maneno, chati, vitabu vyenye maandishi ya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Insha za Kiuamilifu**<br>Shajara | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya shajara, | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya shajara akiwa na mwenzake. | Kwa nini watu hutumia shajara? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (Vipindi 2) | b) kufafanua vipengele vya shajara,<br>c) kuandika shajara akizingatia vipengele vyake,<br>d) kuonea fahari matumizi ya shajara katika maisha ya kila siku. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti maktabani au kusakura mtandao salama akitumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kusoma mifano ya shajara.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na mwenzake shajara aliyoisoma mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza vipengele vya shajara.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika shajara akizingatia vipengele vyake kama vile mambo ya kuandika kwenye shajara, muundo na mtindo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili vipengele vya shajara.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura na kusoma mtandaoni mifano ya shajara kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika mijadala kundini.

**Maadili**

- Uaminifu: mwanafunzi anapoandika matukio ya kweli katika shajara.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu na kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini na kuheshimu maoni ya wenzake kundini.

**Masuala Mtambuko**

- Masuala ya jinsia: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.
- Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.

| |
| --- |
| |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia dhana ya shajara.<br>● Religious Studies na Social Studies: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya kijinsia. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Kielelezo cha shajara, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/kipakatalishi,vitabu vya breli/ vyenye fonti zifaazo, vifa vya kuandikia breli. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Hali za Masharti**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hali ya masharti,<br>b) kutambua matumizi ya hali ya masharti **-nge-** katika matini,<br>c) kutumia hali ya masharti **-nge-** katika matini,<br>d) kutambua matumizi ya hali ya masharti **-ngali-** katika matini,<br>e) kutumia hali ya masharti **-ngali-** katika matini,<br>f) kuchangamkia matumizi yafaayo ya hali ya masharti - | ● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi au maktabani maana ya hali ya masharti.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua matumizi sahihi ya hali ya **-nge-** katika sentensi au vifungu vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua matumizi sahihi ya hali ya **-nge-** katika sentensi au vifungu vyenye maandishi ya breli akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-nge-** kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa | Je, hali ya masharti hutumika vipi? |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **nge-** na **-ngali-** ili kukuza ufasaha wa lugha. | kuzikolezea wino au kuzipigia mstari. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali ya **-nge-** kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kuonyesha matumizi ya hali ya **-nge-** akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua matumizi sahihi ya hali -**ngali-** katika matini yenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza akishirikiana na wenzake katika kikundi. Mwanafunzi asiyeona atambue matumizi sahihi ya hali -**ngali-** katika matini yenye maandishi ya breli akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kuonyesha matumizi sahihi ya hali -**ngali-.**<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali -**ngali-** kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kwa kukoleza wino au kuzipigia mstari akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya hali -**ngali-** kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki akishirikiana na wenzake. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi atafiti matumizi ya hali **-nge-** na **-ngali-** mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuwawasilishia wenzake ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na Ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua hali ya –nge- na -ngali-.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kwa kutumia hali ya -nge- na -ngali-.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua hali ya -nge- na -ngali- na kuzitungia sentensi sahihi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia hali mbalimbali.
- Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya kijinsia.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno, michoro, chati, vifaa vya breli.

| 6.0 USALAMA BARABARANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Kusikiliza kwa Kufasiri**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kusikiliza kwa kufasiri ili kuibanisha,<br>b) kueleza msimamo na mielekeo kuhusu ujumbe wa matini ya kusikiliza,<br>c) kulinganisha misimamo na mielekeo ya ujumbe wa matini aliyosikiliza na ile ya jamii yake kuhusu suala husika,<br>d) kujenga mazoea ya kutambua msimamo na mielekeo katika matini mbalimbali ili kupata maana ya ujumbe. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi au maktabani maana ya kusikiliza kwa kufasiri.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na wenzake matokeo ya utafiti wake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe katika matini andishi au ya kidijitali anayosikiliza kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi asikilize habari kuhusu suala lengwa katika kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuchambua misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake katika kulinganisha misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe wa matini aliyosikiliza na misimamo na mielekeo ya jamii yake kuhusu suala lililozungumziwa katika matini hiyo inayofaa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa muhtasari wa habari aliyoisikiliza kuhusu suala lengwa huku wakichanganua misimamo na mielekeo ya msimulizi /msemaji kuhusu masuala yanayozungumziwa.<br>● Mwanafunzi awaeleze wenzake misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe katika matini andishi au ya | Kwa nini ni muhimu kuwa na misimamo katika matini ulizowahi kusikiliza ? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kidijitali aliyosikiliza kwa maneno yake mwenyewe na kuwataka waangazie vipengele vilivyotumiwa kuonyesha misimamo na mielekeo hiyo<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na mzazi au mlezi wake kuhusu misimamo na mielekeo ya jamii yake kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili na wenzake misimamo na mielekeo katika matini.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza habari.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochanganua misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe na kuihusisha na mielekeo ya jamii yake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwaelezea wenzake misimamo na mielekeo kuhusu ujumbe katika matini aliyosikiliza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojadili na mzazi au mlezi wake kuhusu misimamo na mielekeo ya jamii yake kuhusu ujumbe.

**Maadili**

- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kwa utulivu mielekeo na msimamo kuhusu suala linalozungumziwa.

**Masuala Mtambuko**
Suala la usalama: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kuchanganua habari kwenye matini aliyosikiliza.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusikiliza na kufasiri.
- Creative Arts and Sports na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya usalama.

| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia** |
|---|
| Chati, michoro na picha, mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video), mti maneno, kapu maneno, vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>Ushairi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maudhui na dhamira katika fasihi,<br>b) kueleza maudhui katika shairi,<br>c) kutambua dhamira katika shairi,<br>d) kuchambua shairi kwa kuzingatia maudhui na dhamira,<br>e) kuchangamkia usomaji wa kina wa mashairi ili kupata ujumbe wake. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti maktabani au mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi maana ya maudhui na dhamira.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na wenzake matokeo ya utafiti wake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili maudhui katika shairi alilolisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufafanua dhamira ya shairi alilolisoma.<br>● Mwanafunzi awaelezee wenzake dhamira ya shairi alilolisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuchambua shairi kwa kuzingatia maudhui na dhamira.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, magazetini au vitabuni vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza na kuyachambua kwa kuzingatia dhamira na maudhui ya shairi kisha awatumie wenzake wayatolee maoni. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia | 1. Je. unaweza kueleza maudhui na dhamira katika shairi kivipi?<br>2. Kwa nini ni muhimu kuzingatia maudhui na dhamira katika kuchambua mashairi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | saidizi, au vitabuni vyenye maandishi ya breli na kuyachambua kwa kuzingatia dhamira na maudhui ya shairi kisha awatumie wenzake wayatolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia kujadili maudhui na dhamira ya shairi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura kwenye mitandao kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi salama ili kutafiti kuhusu maudhui ya ushairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojitolea kufanya utafiti maktabani na mtandaoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilishia wenzake maudhui na dhamira ya ushairi. Haiba yake inajengeka zaidi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili maudhui na dhamira ya ushairi. Pia anapowakosoa wenzake kwa upole na kuthamini hoja zao.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafiti kuhusu maudhui na dhamira ya ushairi maktabani na mtandaoni anawajibikia majukumu aliyopewa.
- Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kwa heshima kuhusu uwasilishaji wa wenzake ili kuwakosoa au kuwatia motisha.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposoma shairi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa kina.
- Creative Arts and Sports na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya usalama.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

| |
|---|
| Kamusi mbalimbali, vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya marejeleo vya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa. |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>Methali<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya insha za methali ili kuipambanua,<br>b) kueleze vipengele vya insha ya methali,<br>c) kuandika insha ya methali kwa kuzingatia vipengele vya uandishi husika, (aliye na upungufu wa kuona)<br>d) kuandika insha ya methali kwa kuzingatia vipengele vya uandishi husika na matumizi ya breli yanayofaa(asiyeona),<br>e) kufurahia kufasiri methali na kuziandikia insha zinazoafiki ili kujenga ubunifu. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya insha za methali akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kielelezo cha insha ya methali akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi ajadiliane na wenzake vipengele vya insha ya methali katika kielelezo cha insha aliyosoma.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika insha ya methali kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha ya methali. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya methali kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha ya methali na matumizi ya breli ifaavyo.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoiandika ili waitolee maoni. | Utaandika vipi insha ya methali? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadiliana kuhusu insha za methali.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi yenye teknolojia saidizi kuandika insha hizo za methali na kuzisambaza kwa mtandao.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya methali. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Masuala ya usalama barabarani: mwanafunzi anapoandika insha ya methali kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha.<br>● Creative Arts and Sports na Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya usalama. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya methali, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Vielezi vya Namna** na **vya Wakati**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vielezi vya namna katika matini,<br>b) kutumia vielezi vya namna ipasavyo katika matini,<br>c) kutambua vielezi vya wakati katika matini,<br>d) kutumia vielezi vya wakati ipasavyo katika matini,<br>e) kuchangamkia kutumia vielezi vya namna na vya wakati katika matini. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa vielezi vya namna kutoka kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuorodhesha na kuandika vielezi vya namna kutoka kwenye, kadi maneno, kapu maneno zilizo maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuvipigia mstari vielezi vya namna katika sentensi na vifungu akiwa na wenzake katika kikundi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuviandika kwa italiki vielezi vya namna katika sentensi na vifungu akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutenga vielezi vya namna katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kwa kuvikolezea wino akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga vielezi vya namna katika orodha ya | 1. Kwa nini ni muhimu wa kutambua vielezi namna?<br>2. Vielezi hutumiwa vipi katika matumizi ya lugha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuviandika kwa italiki akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi atunge sentensi au vifungu kwa kutumia vielezi vya namna akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa vielezi vya wakati kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuorodhesha na kuandika vielezi vya wakati kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno zilizo na maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuvipigia mstari vielezi vya wakati katika sentensi na vifungu akiwa na wenzake katika kikundi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuviandika kwa italiki vielezi vya wakati katika sentensi na vifungu akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutenga vielezi vya wakati katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuvikolezea wino akishirikiana na | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga vielezi vya wakati katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuviandika kwa italiki akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vielezi vya wakati akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake sentensi alizozitunga akitumia vielezi vya namna na vya wakati. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua vielezi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia vielezi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa akizingatia matumizi sahihi ya vielezi.

| Uhusiano na Masomo Mengine |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia vielezi.<br>● Creative Arts and Sports na Agriculture: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya usalama. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno, chati/ kadi za breli, |

**7.0 HUDUMA KATIKA ASASI ZA KIJAMII**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Kusikiliza kwa Kutathmini**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini ili kuibainisha,<br>b) kufafanua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini,<br>c) kutathmini ujumbe wa mzungumzaji,<br>d) kutathmini mtazamo wa msemaji kuhusu anachokizungumzia<br>e) kueleza maana ya msamiati kama ulivyotumiwa katika matini aliyosikiliza | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini ili kuubainisha akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini kutoka kwenye mazungumzo mafupi, akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi asikilize mazungumzo kuhusu suala lengwa kutoka vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia | Utatambua vipi ikiwa mzungumzaji anasema ukweli? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | f) kuchangamkia kushiriki katika kusikiliza kwa kuchanganua ili kuboresha mawasiliano. | saidizi huku akijadili vipengele vya kusikiliza kwa kutathmini vilivyozingatiwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa maoni kuhusu suala linaloshughulikiwa katika kauli au kifungu alichokisikiliza.<br>● Mwanafunzi asikilize matini kuhusu suala lengwa kutoka kwenye kinasa sauti au kwa mgeni mwalikwa na kueleza maana ya msamiati ambao umetumiwa katika matini hiyo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikilizia mazungumzo.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa mtazamo wake kuhusu suala alilolisikiliza. Pia anapofasiri maana kutokana na viziada lugha kama vile ishara za uso, toni au kiimbo kinachofaa .

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya huduma kwa jamii: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya ujifunzaji wa kusikiliza kwa kutathmini kuhusu suala lengwa.

| **Uhusiano na Masomo Mengine** |
|---|
| ● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia dhana ya usikilizaji.<br>● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Chati, michoro na picha, mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7 .2.1 Ufupisho**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ufupisho ili kuupambanua,<br>b) kufafanua vipengele vya ufupisho wa kifungu,<br>c) kufupisha kifungu akizingatia vipengele vya ufupisho,<br>d) kujenga mazoea ya kuwasiliana kwa maelezo mafupi. | ● Mwanfunzi aelekezwe kufafanua maana ya ufupisho na kuwaeleza wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya kuzingatia katika kufupisha habari ya kifungu akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi, breli au ya kidijitali akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufupisha kifungu alichokisoma kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusakura vifungu mbalimbali mtandaoni kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na | Je, utajieleza vipi unapotaka kueleza jambo kwa ufupi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuvifupisha kwa kuzingatia vipengele vya ufupisho.<br>● Mwanafunzi amsome mwenzake kifungu alichofupisha akizingatia vipengele vya ufupisho ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotambua na kujadili vipengele vya kuzingatia katika kufupisha kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura vifungu mbalimbali mtandaoni kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuvifupisha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kusakura vifungu mbalimbali na kuvifupisha.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofupisha kifungu na kuwasomea wenzake.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapohusishwa katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kufupisha kifungu.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya shughuli za huduma kwa jamii: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa kina.
- Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii.

| |
|---|
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br><br>Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya marejeleo vya breli, vitabu vyenyefonti inayofaa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Insha za Kubuni** Maelezo<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika insha ya maelezo,<br>b) kueleza umuhimu wa kutumia lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika insha ya maelezo,<br>c) kutumia ipasavyo lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika kuandika insha ya maelezo,<br>d) kutumia ipasavyo lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika kuandika insha ya | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua lugha inayoathiri hisi katika insha ya maelezo kutoka kwa vielelezo vya insha kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali zenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua jinsi matumizi ya lugha katika insha ya maelezo yanavyoathiri hisia mbalimbali.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kupigia mstari lugha iliyotumiwa kuathiri hisia katika kielelezo cha insha ya maelezo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika kwa italiki maneno yanayoathiri hisia katika kielelezo cha insha ya maelezo akitumia breli ifaavyo.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua umuhimu wa lugha inayoathiri hisia kutokana na kifungu kwenye kitabu chenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknlojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona | Je, mbona ni muhimu kutumia lugha inayoathiri hisia mbalimbali katika insha ya maelezo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | maelezo na matumizi ya breli yafaayo,<br>e) kufurahia kuandika insha yenye maelezo yanayojenga picha dhahiri. | aelekezwe kutambua umuhimu wa lugha inayoathiri hisia kutokana na kifungu kwenye kitabu chenye maandishi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanfunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia lugha inayoathiri hisia mbalimbali, matumizi ya breli yanayostahili na kutekeleza majukumu ya kushawishi, kuburudisha, kupasha habari au kufunza.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha ya maelezo aliyoandika ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kupigia mstari lugha inayoonyesha hisia au kuandika maeneno yanayoathiri hisia.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha inayotumia lugha yenye kuathiri hisia za msomaji.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha aliyoandika.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya shughuli za huduma kwa jamii: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.

| Uhusiano na Masomo Mengine |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English, Indigenous Languages na Foreign Languages: masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha.<br>● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/kipakatalishi, kielelezo cha insha ya maelezo, vifaa vya kuandikia breli, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo na rangi zisizotatiza. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Vielezi vya Mahali** na **vya Idadi**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vielezi vya mahali katika matini,<br>b) kutumia vielezi vya mahali ipasavyokatika matini,<br>c) kutambua vielezi vya idadi katika matini,<br>d) kutumia vielezi vya idadi ipasavyo katika matini,<br>e) kuchangamkia kutumia vielezi vya mahali na vya idadi katika sentensi na vifungu. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa vielezi vya mahali kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya vielezi vya mahali kisha aelekezwe kuviandika kwenye karatasi ya breli, kadi maneno, kapu maneno zilizo na maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuvipigia mstari vielezi vya mahali katika sentensi na vifungu akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuviandika kwa italiki vielezi vya mahali katika sentensi na vifungu akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutenga vielezi vya mahali katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na fonti | 1. je, vielezi vya mahali hutumiwa vipi?<br>2. Vielezi vya mahali na vya idadi hutofautianaje? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga vielezi vya mahali katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, karatasi ya breli kwa kuviandika kwa italiki.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vielezi vya mahali.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake sentensi alizozitunga ili watambue vielezi vya mahali.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa vielezi vya idadi kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya maneno na aelekezwe kuandika vielezi vya idadi kwenye, kadi maneno, kapu maneno zilizo na maandisshi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuvipigia mstari vielezi vya idadi katika sentensi na vifungu akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika kwa italiki vielezi vya idadi katika sentensi na vifungu akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutenga vielezi vya idadi katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | teknolojia saidizi kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga vielezi vya idadi katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuviandika kwa italiki.<br>● Mwanafunzi atunge sentensi au vifungu kwa kutumia vielezi vya idadi.<br>● Mwanafunzi amsomea mwenzake sentensi alizozitunga ili atambue vielezi vya idadi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua vielezi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vielezi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vielezi na kuvitungia sentensi sahihi na vifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake vielezi vinavyohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Masuala ya huduma kwa jamii: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia vielezi.

| |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia vielezi.<br>● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno, chati, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo na rzngi zisizotatiza, |

| **8.0 MISUKOSUKO YA KIJAMII** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Uzungumzaji wa Kushawishi**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya uzungumzaji wa kushawishi ili kuupambanua,<br>b) kubainisha miktadha ya uzungumzaji wa kushawishi,<br>c) kutambua vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji wa kushawishi, | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleze maana ya uzungumzaji wa kushawishi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kubainisha, miktadha katika jamii yake ambamo uzungumzaji wa kushawishi hutokea.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji wa kushawishi.<br>● Mwanafunzi abuni mazungumzo mepesi kuhusu suala lengwa na kuwawasilishia wenzake wamtathmini iwapo ametumia | 1. Mbona ni muhimu kubainisha miktadha ya uzungumzaji wa kushawishi?<br>2. Utashawishi vipi wengine kwa mazungumzo yako? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kufanya mazungumzo ya kushawishi akizingatia vipengele vya uzungumzaji wa kushawishi,<br>e) kujenga mazoea ya kuwasilisha hoja kwa mazungumzo yanayoshawishi hadhira. | vipengele vifaavyo vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa kushawishi.<br>● Mwanafunzi asikilize uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa kutoka kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi au mgeni mwalikwa na kubainisha vipengele vya uzungumzaji wa kushawishi vilivyozingatiwa.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake katika uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa huku akizingatia vipengele vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa kushawishi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojieleza kuhusu suala lengwa kwa njia wazi na kwa lugha inayomwaminisha msikilizaji kwamba anasema ukweli.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa na kuyawasilisha kwa mtindo ufaao.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kushawishi kuhusu suala lengwa.

**Maadili**

- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza bila kuwakatiza au kushughulikia mengine wanapozungumza.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika kujifunza.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake na kutoa mchango katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhiriki na wengine katika mazungumzo ya kushawishi kuhusu suala lengwa kwa utulivu.

**Masuala Mtambuko**

Suala la misukosuko ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki uzungumzaji wa kushawishi kuhusu suala lengwa.

| **Uhusiano na Masomo Mengine** |
| --- |
| ● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia stadi ya kuzungumza.<br>● Social Studies: somo hili linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video), vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli. |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>Ushairi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mandhari katika fasihi,<br>b) kutambua mandhari mbalimbali katika shairi,<br>c) kueleza umuhimu wa mandhari katika shairi,<br>d) kufafanua vipengele vya muundo katika shairi,<br>e) kuchambua shairi kwa kuzingatia mandhari na muundo,<br>f) kuchangamkia nafasi ya mandhari na muundo katika shairi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi au maktabani maana ya mandhari katika fasihi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na wenzake matokeo ya utafiti wake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma mashairi mbalimbali ili kutambua mandhari mbalimbali katika shairi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza umuhimu wa mandhari katika shairi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufafanua vipengele vya muundo wa shairi ili kuipambanua.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kughani shairi ili kutambua mandhari na muundo katika shairi. | 1. Je, utatambua vipi mandhari katika mashairi uliyoyasoma?<br>2. Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele vya muundo katika shairi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kuchambua shairi alilolisoma na kubainisha mandhari na muundo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotambua na kujadili mandhari na muundo kwenye shairi akiwa na wenzake katika kikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua shairi na kubainisha mandhari na muundo wa shairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti maktabani au mtandaoni kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuhusu muundo na mandhari katika shairi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili kuhusu mandhari na muundo katika shairi.
- Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kuhusu uwasilishaji wa wenzake ili kuwarekebisha au kuwahimiza.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki kukariri shairi kuhusu suala lengwa.

**Masuala Mtambuko**
Suala la misukosuko ya kijamii: mwanafunzi anaposoma shairi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa kina.
- Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

| |
|---|
| Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya marejeleo vya breli, vitabu vyenye fonti inayofaa |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Viakifishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya mabano na kistari kifupi katika matini,<br>b) kutumia mabano na kistari kifupi ipasavyo katika matini,<br>c) kutumia alama ya mabano na kistari kifupi za breli ipasavyo katika matini ya breli(asiyeona),<br>d) kujenga mazoea ya kutumia ipasavyo mabano na kistari kifupi katika matini ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua matumizi ya mabano na kistari kifupi katika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kwenye matini andishi, ya breli na za kidijitali zilizo na teknolojia saidizi..<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kundika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kuhusu suala lengwa akitumia mabano na kistari kifupi ipasavyo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kuhusu suala lengwa akitumia nukta nundu zinazounda alama ya mabano na kistari kifupi ipasavyo.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuaandika kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, kifungu kifupi kwa kutumia mabano na kistari kifupi ipasavyo na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili wakitolee maoni. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuaandika kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, kifungu | 1. Je, mabano hutumiwa vipi katika matini?<br>2. Je, kistari kifupi hutumiwa vipi katika matini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kifupi kwa kutumia nukta nundu zinazounda mabano na kistari kifupi ipasavyo na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili wakitolee maoni.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kusahihisha kifungu ambacho hakijatumia mabano na kistari kifupi ipasavyo.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake kifungu alichoandika na kuwataka waandike maneno, sentensi au vifungu vinavyostahili kuwa na mabano na kistari kifupi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili matumizi ya mabano na kistari kifupi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika kifungu na kukisambaza mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya mabano na kistari kifupi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
**Suala la misukosuko ya kijamii**: mwanafunzi anapotunga sentensi au vifungu kuhusu suala lengwa akitumia mabano na kistari kifupi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia uakifishaji.

| |
|---|
| ● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Kielelezo cha viakifishi mabano na kistari kifupi, tarakilishi/kipakatalishi, nakala ya kifungu kilicho na alama za uakifishaji, Kielelezo cha matumizi ya mabano na kistari kifupi, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo, |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA katika matini,<br>b) kutambua upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-ZI na YA-YA katika sentensi,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA katika matini kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia upatanisho ufaao wa ngeli ya U-ZI na YA-YA ili kujenga ufasaha wa lugha. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa nomino za ngeli ya U-ZI kwenye chati, kadi za maneno, kapu maneno zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya nomino za ngeli ya U-ZI kwenye karatasi ya breli, kadi za maneno, kapu maneno zilizo na maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kisha aziorodheshe.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya U-ZI katika sentensi na mafungu ya maneno yenye fonti ifaayo akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya U-ZI katika sentensi na mafungu ya maneno yenyemaandishi ya breli akishirikiana na wenzake. | 1. Kwa nini ni muhimu kuzingatia upatanisho wa kisarufi katika ngeli ya U-ZI na YA-YA?<br>2. Utatumia vipi vitu uvijuavyo vyenye majina yaliyo katika ngeli ya U-ZI na YA -YA? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kuunda sentensi akitumia majina katika ngeli ya U-ZI ili kubainisha upatanisho wa kisarufi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuorodhesha majina katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya U-ZI akiwa na wenzake katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutenga nomino za ngeli ya U-ZI katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga nomino za ngeli ya U-ZI katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa nomino za ngeli ya YA-YA kwenye chati, kadi za maneno, kapu maneno zilizo na fonti zifaazo na rani zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya nomino za ngeli ya YA-YA kwenye chati, kadi za maneno, kapu maneno yenye maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kisha aziandike.. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya YA-YA katika sentensi na mafungu ya maneno akishirikiana na wenzake<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuunda sentensi akitumia majina katika ngeli ya YA-YA ili kubainisha upatanisho wa kisarufi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuorodhesha majina katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya YA-YA akiwa na wenzake katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutenga nomino za ngeli ya YA-YA katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rani zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga nomino za ngeli ya YA-YA katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu vyenye maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki.<br>• Mwanafunzi amtajie mzazi au mlezi wake majina ya vitu vilivyo katika ngeli ya U-ZI na YA-YA katika mazingira ya nyumbani. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA na kuzitungia sentensi sahihi na vifungu.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA katika mazingira ya nyumbani. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Suala la misukosuko ya kijamii: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za ngeli ya U-ZI na YA-YA. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia upatanisho wa kisarufi.<br>● Social Studies: somo hili linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi rununu, projekta, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno, michoro, chati/kadi za breli, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo, |

| 9.0 MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA BIASHARA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti **/j/** na **/nj/** katika maneno ipasavyo,<br>b) kutamka maneno yenye sauti **/j/** na **/nj/**,<br>c) kubuni vitanzandimi vinavyohusisha sauti /**j** /na /**nj/,**<br>d) kuchangamkia matamshi bora ya sauti **/j/** na **/nj/** ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua sauti **/j/** na **/nj/** katika maneno.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kusikiliza vitanzandimi katika kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kutambua maneno yenye sauti **/j/** na **/nj/** na kuyatamka ipasavyo<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kutamka vitanzandimi vyepesi vinavyohusisha matamshi ya sauti/ **j/** na /**nj/.**<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kusikiliza vitanzandimi katika kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kutambua maneno yenye sauti **/j/** na **/nj/** na kuyatamka ipasavyo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kubuni vitanzandimi vinavyohusisha sauti **/j/** na **/nj/** na kuvikariri kwa wenzao.<br>● Mwanafunzi ashiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /**j/** na /**nj/.** | Kwa nini ni muhimu kutambua sauti /**j/** na /**nj/** katika maneno? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua sauti /j/ na /nj/ katika maneno.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kusikiliza vitanzandimi vyenye sauti /j/ na /nj/.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni vitanzandimi vyepesi akitumia maneno yenye sauti /j /na /nj/.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti lengwa na anapochangia katika kazi ya kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na mzazi/mlezi kwa kuhusisha matamshi bora ya sauti /**j** /na / **nj/.**

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapotamka na kutofautisha sauti lengwa katika maneno yanayohusiana na biashara.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia dhana ya kutofautisha na kutamka sauti.
- Pre-technical Studies: somo hili pia linashughulikia ujuzi wa kidijitali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta), vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli, vifaa vya kuandikia breli,

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Ufahamu wa Kifungu cha Kushawishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha kushawishi,<br>b) kueleza maana za maneno kama yalivyotumiwa katika kifungu cha kushawishi,<br>c) kuchangamkia usomaji wa ufahamu wa kifungu cha kushawishi ili kukuza hamu ya ujifunzaji. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu chenye maandishi ya breli cha kushawishi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha kushawishi ili kubainisha matumizi ya lugha shawishi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kumtungia mwenzake sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma ili kubainisha matumizi ya lugha shawishi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujibu maswali kutokana na kifungu cha kushawishi alichokisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa muhtasari wa kifungu cha kushawishi alichokisoma na kuwasambazia wenzake mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi ili wakitolee maoni.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuhusu matini zinazoshughulikia suala lengwa. | Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele mbalimbali unaposoma kifungu cha kushawishi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapohakiki sentensi zilizotungwa na wenzake kwa kutumia msamiati wa suala lengwa na kutoa maoni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoweza kusakura tovuti kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi ili kutafuta matini lengwa na kuisoma kwa kuzingatia maadili. Vilevile, anapoandika muhtasari kwa kutumia kifaa cha kidijitali na kuwatumia wenzake.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata matini mbalimbali na kuzisoma akizingatia maadili katika usomaji wa kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anapohakiki sentensi zilizotungwa na wenzake kwa kutumia msamiati wa suala lengwa na kutoa maoni yake.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapotathmini maoni ya wenzake wanapojadili sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali zinazofaa kusomwa. Pia anapowakosoa wenzake kwa kwa upole.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kwa kuvitunza ipasavyo na kuzingatia maadili.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali zinazofaa kusomwa.
- Uadilifu: mwanafunzi anapochagua matini faafu mtandaoni kwa mujibu wa sifa zinazofaa kuzingatiwa katika uteuzi wa matini husika.

**Masuala Mtambuko**
Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapopata maarifa mtandaoni kuhusu matumizi ya vifaa vya kidijitali katika biashara.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kidijitali.
- Pre-technical Studies: somo hili pia, linashughulikia ujuzi wa kidijitali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa,

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha za Kubuni** Masimulizi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya ukuzaji wa wazo baina ya aya za insha ya masimulizi,<br>b) kueleza ukuzaji wa wazo baina ya aya za insha ya masimulizi,<br>c) kuandika insha ya masimulizi inayozingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya,<br>d) kuandika insha ya masimulizi ya breli inayozingatia matumizi ya mikato, alama za uakifishaji, herufi kubwa za breli na kukuzaji wa wazo baina ya aya, (asiyeona)<br>e) kufurahia kuandika insha za masimulizi zinazozingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya ukuzaji wa wazo baina ya aya za insha ya masimulizi kwenye matini za kimaandishi, breli au za kidijitali zilizo na teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza jinsi wazo lilivyokuzwa baina ya aya za insha ya masimulizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika vidokezo vya insha vinavyozingatiwa kwa kukuza wazo baina ya aya akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuonaaelekezwe kuandika insha ya masimulizi akizingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya na kusaidiana na wenzake kuisahihisha. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya masimulizi akizingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya kwa kutumia breli ipasavyo na kusaidiana na wenzake kuisahihisha.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi ili waitolee maoni.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kusahihisha insha ya maelezo aliyoandika kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia ukuzaji wa wazo baina ya aya. | Je, unawezaje kulikuza wazo baina ya aya za insha ya masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi amsomee mzazi, mlezi wake au mwenzake aya aliyoandika ili kutoa maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kusahihisha insha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusambazia insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapolikuza wazo baina ya aya za insha katika utungo wake kwa ufasaha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika na kuwasomea wenzake insha.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko**
Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapoandika insha inayohusisha maudhui ya biashara.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia, yanashughulikia uandishi wa insha.
- Pre-technical Studies: somo hili pia, linashughulikia ujuzi wa kidijitali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Kielelezo cha insha ya masimulizi, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/kipakatalishi, vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo na rangi zisizotatiza, vifaa vya kuandikia breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika matini,<br>b) kutambua upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika matini,<br>c) kutumia ipasavyo upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika matini,<br>d) kuchangamkia matumizi yafaayo ya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya PA-KU-MU katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU kwenye chati, kadi za maneno, kapu la maneno zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona apewe orodha ya nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU kwenye kadi za maneno, kapu la maneno zilizo na maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kisha kuziorodhesha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU katika sentensi au vifungu akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu vyenye upatanisho ufaao wa kisarufi kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma matini au kusakura kwenye mtandao kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kutafuta maneno yenye majina yaliyo katika ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU.<br>● Mwanafunzi amweleze mzazi, mlezi au mwenzake sentensi alizozitunga akitumia majina katika ngeli za LI, KU na PA-KU-MU ili kutoa maoni. | Ni vipi tunatumia upatanisho wa kisarufi katika ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU?<br><br>. |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughjuli za ujifunzaji. | | | | |

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya teknolojia vyenye teknolojia saidizi katika kutambua nomino katika ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino za ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU na kuzitungia sentensi na vifungu vyenye upatanisho ufaao wa kisarufi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma matini au kusakura kwenye mtandao kutafuta maneno yenye viambishi vya ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji, pia anapojitolea kufanya kazimradi.
- Umoja na upendo: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko**

Elimu ya matumizi ya fedha: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino ngeli ya LI, KU na PA-KU-MU.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia upatanisho wa kisarufi.
- Pre-technical Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya biashara.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi, rununu, kapu maneno, mti maneno, kadi maneno, michoro, chati, vifaa vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo,

| 10.0 KUKABILIANA NA MSONGO WA MAWAZO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi lililopendekezwa** |
| **10 .1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Mazungumzo:** Malumbano ya Utani<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya malumbano ya utani kama kipera cha mazungumzo,<br>b) kueleza sifa za malumbano ya utani,<br>c) kutambua vipengele vya uwasilishaji wa malumbano ya utani,<br>d) kuwasilisha malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vya uwasilishaji,<br>e) kuchangamkia uwasilishaji wa malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi katika uwasilishaji. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya malumbano ya utani akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili sifa za malumbano ya utani akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kimsingi vya uwasilishaji wa malumbano ya utani.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza malumbano ya utani katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au kutoka kwa mgeni mwalikwa au mwalimu na kutambua vipengele vya kimsingi katika uwasilishaji.<br>● Mwanafunzi awasilishe malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi katika uwasilishaji wake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwaelezea wenzake namna ya kuwasilisha malumbano ya utani kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi katika uwasilishaji.<br>● Mwanafunzi amweleze mzazi au mlezi jinsi ya kuwasilisha malumbano ya utani kwa | Kwa nini tunazingatia vipengele vya uwasilishaji wa malumbano ya utani tunapozungumza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuzingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasilisha mazungumzo kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi vya mazungumzo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowaeleza wenzake namna ya kuwasilisha mazungumzo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza malumbano ya utani.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua vipengele vya kimsingi vya mazungumzo aliyosikiliza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomweleza mzazi au mlezi jinsi ya kuwasilisha malumbano ya utani.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Masuala ya afya: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kuwasilisha malumbano ya utani kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia, yanashughulikia tungo za fasihi simulizi.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

Chati, mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta), mti maneno, kapu maneno, vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>Ushairi<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya wahusika katika fasihi,<br>b) kutambua wahusika katika shairi,<br>c) kueleza sifa za wahusika katika shairi,<br>d) kuchambua shairi kwa kuzingatia sifa za wahusika,<br>e) kujenga mazoea ya kuchambua wahusika katika mashairi ili kuimarisha uwazaji wa kina. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi au maktabani maana ya wahusika katika fasihi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua wahusika *(k.v. nafsineni)* katika shairi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuchambua wahusika katika shairi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na wenzake sifa za wahusika katika shairi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchambua shairi na kutaja sifa za nje za wahusika kutokana na sura au umbo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchambua shairi na kutaja sifa za nje za wahusika kutokana maelezo ya sura au umbo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza wahusika katika mashairi akiwa na wenzake ili kukuza uelewa wa sifa zao.<br>● Mwanafunzi amsome mzazi au mlezi wake shairi na kujadiliana naye kuhusu wahusika. | Tunachambua vipi wahusika waliopo katika mashairi uliyowahi kusoma? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma mashairi akiwa na wenzake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kusoma mashairi kwa mahadhi yafaayo katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika usomaji wa shairi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza wahusika katika mashairi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua wahusika katika mashairi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi mashairi na kujadiliana naye kuhusu wahusika.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya afya: kutokana na ujumbe wa shairi kuhusu suala lengwa.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika majadiliano ya uchambuzi wa mashairi katika kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa kina.
- Integrated Science: masomo haya yanashughulikia masuala ya msongo wa mawazo.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya breli, vitabu vya marejeleo yenye fonti zinazofaa

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Barua ya Kuomba Kazi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya barua rasmi ya kuomba kazi,<br>b) kutambua vipengele vya barua rasmi ya kuomba kazi,<br>c) kuandika barua rasmi ya kuomba kazi akizingatia vipengele vyake, (aliye na upungufu wa kuona)<br>d) kuandika barua rasmi ya kuomba kazi akizingatia vipengele vyake akitumia breli(asieona),<br>e) kujenga mazoea ya kuandika barua rasmi ya kuomba kazi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya barua rasmi ya kuomba kazi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya barua rasmi ya kuomba kazi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua ujumbe unaoafiki barua rasmi ya kuomba kazi kwa kujadiliana na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua na kutumia lugha inayofaa kwa uandishi wa barua rasmi ya kuomba kazi kwa kujadili na wenzake. Mwanafunzi asiyeona atambue na atumie lugha inayofaa kwa uandishi wa barua rasmi ya breli ya kuomba kazi kwa kujadili na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili kwa madhumuni ya kufahamu muundo wa barua rasmi ya kuomba kazi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika barua rasmi ya kuomba kazi kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kuwasambazia wenzake kupitia mtandao ili waitolee maoni. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika barua rasmi ya kuomba kazi akizingatia sheria za matumizi ya mikato, | Je, ni kwa nini tunazingatia vipengele tunapoandika barua rasmi ya kuomba kazi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | alama za uakifishaji na herufi kubwa za breli kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kuwasambazia wenzake kupitia mtandao ili waitolee maoni.<br>● kumweleza mzazi au mlezi wake namna ya kuandika barua rasmi ya kuomba kazi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadili ujumbe, lugha na muundo wa barua rasmi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika barua na kuisambaza kwa mtandao.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika barua rasmi ya kuomba kazi.
- Hamu ya ujifunzaji**:** mwanafunzi anapomwelezea mzazi au mlezi wake namna ya kuandika barua rasmi ya kuomba kazi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Masuala ya afya: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili ujumbe, lugha na muundo wa barua rasmi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia barua rasmi.
- Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya msongo wa mawazo.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

| |
|---|
| Kielelezo cha barua ya kuomba kazi, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/kipakatalishi,vitabu vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo, vifaa vya kuandikia breli, |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vihusishi**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya vinyume vya vihusishi,<br>b) kutambua vinyume vya vihusishi katika matini,<br>c) kutumia vinyume vya vihusishi ipasavyo katika matini,<br>d) kujenga mazoea ya kutumia ipasavyo vinyume vya vihusishi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya vinyume vya vihusishi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua matumizi sahihi ya vinyume vya vihusishi kutoka katika vitabu vyenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi au chati yenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza akiwa na wenzake au katika kikundi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua matumizi sahihi ya vinyume vya vihusishi kutoka katika vitabu vyenye maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake au katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kuonyesha matumizi ya vinyume vya vihusishi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua sentensi | 1. Kwa nini ni muhimu kutambua vinyume vya vihusishi katika matini?<br>2. Unatamia vipi vinyume vya vihusishi katika matini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | zinazoashiria matumizi ya vinyume vya vihusishi kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya vinyume vya vihusishi kutokana na mchanganyiko wa sentensi kutoka katika vitabu vyenye maandishi ya breli, tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuziandika kwa italiki.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi, mlezi au mwenzake sentensi zenye vihusishi na vinyume vyake vinavyotokea katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua vinyume vya vihusishi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha vinyume vya vihusishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vinyume vya vihusishi na kuvitungia sentensi sahihi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua au kutunga sentensi sahihi kuhusu vinyume vya vihusishi.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Kukabiliana na msongo wa mawazo: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia vinyume.<br>● Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya msongo wa mawazo. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi, chati, vifaa vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo, |

| **11.0 HAKI ZA KIBINADAMU** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **11.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **11.1.1 Uzungumzaji katika Sherehe**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya uzungumzaji katika sherehe,<br>b) kutambua miktadha katika jamii ambapo uzungumzaji katika sherehe hufanywa,<br>c) kufafanua ujumbe tofautitofauti unaoafiki uzungumzaji katika miktadha mbalimbali ya sherehe,<br>d) kueleza vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji katika muktadha wa sherehe,<br>e) kutoa mazungumzo katika muktadha wa sherehe kwa kutumia vipengele vifaavyo,<br>f) kuchangamkia mazungumzo yafaayo katika miktadha ya sherehe. | • Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya uzungumzaji katika sherehe akishirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua miktadha katika kijamii yake ambamo uzungumzaji katika miktadha ya sherehe hufanywa akishirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusakura katika mtandao kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kutafiti ujumbe unaoafiki uzungumzaji katika miktadha mbalimbali ya sherehe akishirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi asikilize uzungumzaji wa aina mbalimbali kutoka kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mwalimu au mgeni mwalikwa na kubainisha ule unaohusu muktadha ya sherehe.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza katika miktadha ya sherehe akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuigiza uzungumzaji katika miktadha ya sherehe | Kwa nini tunazingatia vipengele wakati wa kuzungumza katika muktadha wa sherehe? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | huku akizingatia vipengele vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa aina hii. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza maana ya uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni maigizo kuhusu uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kuigiza uzungumzaji katika muktadha wa sherehe akizingatia vipengele vya uwasilishaji wa uzungumzaji wa aina hii.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadili vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake zamu ya kushiriki katika uzungumzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali alivyotumia kusakura katika mtandao kutafiti ujumbe unaoafiki uzungumzaji katika miktadha ya sherehe.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wengine na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko**
**Uraia**: mwanafunzi anaposhiriki katika uzungumzaji kuhusu haki za binadamu.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia dhana ya uzungumzaji.
- Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya haki za binadamu.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu), vitabu mbalimbali vyenye fonti zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli,

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **11.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kuteua matini ya kusoma ya kiwango chake,<br>b) kueleza ujumbe katika matini ya kujichagulia,<br>c) kutambua maana ya msamiati na matumizi mengine ya lugha katika matini ya kujichagulia,<br>d) kutumia msamiati aliojifunza ipasavyo katika sentensi,<br>e) kufurahia kusoma matini ya kujichagulia ili kujenga ufasaha wa lugha. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchagua matini yenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza ya kiwango chake na kuisoma. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuchagua matini yenye maandishi ya breli ya kiwango chake na kuisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuelezea wenzake ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyoisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia kamusi yenye fonti inayofaa kutafuta maana ya maneno asiyoyajua akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kutafuta maana ya maneno asiyoyajua akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujenga rekodi ya msamiati na matumizi mengine ya lugha aliyojifunza katika kitabu au shajara yake. | 1. Utachagua vipi matini ya kusoma?<br>2. Kwa nini ni muhimu kujichagulia matini ya kusoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa muhtasari wa matini ya kujichagulia aliyoisoma na kuwasilisha kwa wenzake ili waitolee maoni.<br>● Mwanafunzi asakure mtandaoni kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kujichagulia matini ya ziada kisha aisome.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake muhtasari wa matini ya kujichagulia aliyosoma ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyosoma.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoeleza ujumbe wa matini ya kujichagulia akizingatia ufasaha wa lugha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia kwa usahihi msamiati katika matini aliyoisoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kujichagulia matini ya kusoma.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapokubaliana na maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.

| |
|---|
| ● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Masuala ya haki za binadamu: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa mapana.<br>● Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya haki za binadamu. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Kamusi mbalimbali, vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta, vitabu vya marejeleo vya breli, vitabu vyenye fonti zinazofaa, |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.3 Kuandika** | **11.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>Maelezo<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) Kueleza mitazamo katika insha za maelezo,<br>b) kuandika insha ya maelezo akizingatia mtazamo mahususi,<br>*c)* kuandika insha ya maelezo akizingatia mtazamo mahususi akitumia breli,<br>d) kufurahia kuandika insha za maelezo zinazoonyesha mitazamo mahususi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua mitazamo mbalimbali ya kimaelezo katika insha za maelezo akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza mitazamo mbalimbali ya kimaelezo katika insha za maelezo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika vidokezo vya insha vinavyozingatia mitazamo ya kimaelezo atakavyotumia katika insha yake ya maelezo.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuaandika insha ya maelezo akizingatia mitazamo ya kimaelezo aliyochagua kutumia. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika insha ya maelezo akizingatia mitazamo ya kimaelezo aliyochagua kutumia, akitumia breli ipasavyo.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake insha aliyoandika au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi ili waitolee maoni<br>● Mwanafunzi amsomea mzazi au mlezi insha ya maelezo aliyoiandika ili aitolee maoni. | Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele katika kuandika insha ya maelezo? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika insha na kuwasomea wenzake kwa ufasaha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusambazia wenzake insha aliyoiandika.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha yenye mpangilio mzuri wa maelezo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha nzuri na kuwasomea wenzake.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko**

- Masuala ya haki za binadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha.
- Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya haki za binadamu

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

Kielelezo cha insha ya maelezo, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/kipakatalishi, vifaa vya breli, vitabu vyenye fonti zifaazo

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha katika vitenzi,<br>b) kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na Kutendesha ipasavyo katika matini ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vitenzi, viambishi vya kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafuni aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutenga vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha kwenye chati, karatasi za breli, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa na mwenzake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha kwenye vitabu vya breli, orodha maneno, kadi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa na mwenzake<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutenga vitenzi katika kauli ya kutendana kutendeana na kutendesha katika sentensi na vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, tarakilishi yenye teknolojia saidizi, kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutenga vitenzi katika kauli ya kutendana kutendeana na kutendesha | Kwa nini ni muhimu kujifunza kauli za vitenzi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | katika sentensi na vifungu kwenye vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuviandika katika italiki.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kugeuza vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kujaza mapengo kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kujaza mapengo kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi au vifungu kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi amweleze mzazi, mlezi au mwenzake jinsi ya kutumia vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha watoe maoni yao. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kutoa mchango wake katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kutambua vitenzi katika kauli ya kutendana, kutendeana na kutendesha.

- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vitenzi katika kauli ya kutendana kutendeana na kutendesha.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua viambishi vya kauli ya kutendana kutendeana na kutendesha na kuandika vitenzi katika kauli hizo.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko**
Suala la haki za kibinadamu: mwanafunzi anaposhiriki na kutoa mchango wake katika kazi za kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya pia yanashughulikia mnyambuliko wa vitenzi.
- Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia masuala ya haki za binadamu.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi, chati, vitabu vilivyoidhinishwa,kapu maneno, kadi maneno

## 12.0 MAGONJWA YANAYOTOKANA NA MIENENDO YA MAISHA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **12.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza habari katika matini ya kusikiliza,<br>b) kukadiria maana ya msamiati mahususi na vifungu katika matini ya kusikiliza,<br>c) kuchanganua mitazamo na maoni katika kifungu cha kusikiliza,<br>d) kufurahia kusikiliza vifungu vya kusikiliza ili kuimarisha uwezo wa kusikiliza. | ● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kueleza hoja muhimu katika habari aliyoisikiliza kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa au wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kukadiria maana ya msamiati mahususi na vifungu katika matini ya kusikiliza akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili mitazamo na maoni katika kifungu cha kusikiliza akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi ashirikishe mzazi, mlezi au mwenzake kusikiliza kifungu kutoka kifaa cha kidijitali *chenye teknolojia saidizi* na kujadili mitazamo katika kifungu hicho. | Je, kwa nini ni muhimu kusikiliza kwa makini? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika mazungumzo kuhusu suala lengwa.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposikiliza habari, kuichanganua na kutambua hoja muhimu na kuziwasilisha kwa mtindo ufaao.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake kuhusu suala lengwa.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoiwasilisha upya habari aliyosikiliza. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wengine fursa ya kutambua habari za ziada na kuzidondosha bila kuwakatiza.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Masuala ya afya: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika mazungumzo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Languages: masomo haya yanashughulikia stadi ya kusikiliza.<br>● Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yananashughulikia magonjwa mbalimbali. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Mgeni mwalikwa,vitabu mbalimbali vyenye hati zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli,vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.2 Kusoma** | **12.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze<br>a) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>b) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>c) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>d) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>e) kujenga mazoea ya kusoma vifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji matini ufaao ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha.<br><br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame vielelezo vya video za watu wanaosoma kwa ufasaha makala akiwa na wenzake, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusikiliza vielelezo vya video ikiwa na maelezo ya matukio katika video<br><br>inayoonyeshwa za watu wanaosoma kwa ufasaha makala akiwa na wenzake.<br><br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali akizingatia matamshi bora. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu chenye maandishi ya breli kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya | Je, kwa nini ni muhimu kusoma kifungu cha nathari ukizingatia matamshi bora? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kidijitali akizingatia matamshi bora.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona asome kifungu cha habari chenye chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza kwa kasi ifaayo kuhusu suala lengwa. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu cha habari yenye maandishi ya breli kwa kasi ifaayo kuhusu suala lengwa.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo *(k.v. kiwango cha sauti na kiimbo)*<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa akiwa na wenzake katika kikundi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu kwa kwa kutumia toni/kiimbo kifaacho panapofaa akiwa na wenzake katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona awasome wenzake matini mbalimbali zenye fonti zinazofaa vitabuni au katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akizingatia vipengele vya usomaji ufaao ili watoe maoni yao. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi amsome mzazi, mlezi au mwenzake kifungu akizingatia vipengele vya usomaji ufaao ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kueleza vipengele vya usomaji ufaao wa matini.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake matini mbalimbali kwa kuzingatia vipengele vya usomaji bora.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu akizingatia vipengele vya usomaji ufaao.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapochukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya afya: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English na Kenya Sign Languages: masomo haya yanashughulikia kusoma kwa kina.
- Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia magonjwa mbalimbali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, vitabu vya breli, vitabu vyenye hati inayofaa, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.3 Kuandika** | **12.3.1 Hotuba ya Kushawishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kueleza maana ya hotuba ya kushawishi ili kuitofautisha na aina nyingine za hotuba,<br>b) kueleza vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba ya kushawishi,<br>c) kuandika hotuba ya kushawishi akizingatia vipengele vifaavyo,<br>*d) kuandika kwa kutumia breli ipasavyo hotuba ya kushawishi akizingatia vipengele,(asiyeona),*<br>e) kuchangamkia kuandika ipasavyo hotuba ya kushawishi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya hotuba ya kushawishi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua hotuba ya kushawishi katika matini au kifaa cha breli chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa hotuba ya kushawishi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kielelezo cha hotuba ya kushawishi na kujadili vipengele vilivyotumiwa katika hotuba hiyo akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na wenzake vidokezo vinavyoweza kutumiwa katika kuandika hotuba ya kushawishi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika hotuba ya kushawishi kuhusu suala lengwa akitumia vidokezo walivyovijadili. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kandika hotuba ya kushawishi kuhusu suala lengwa akitumia vidokezo walivyovijadili na kuzingatia matumizi yanayostahili ya breli. | Utawashawishi vipi wasomaji wakati wa kutoa hotuba? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi awasomee wenzake hotuba yake au kuwasambazie kupitia mtandao ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadili vipengele vya kuzingatia katika kuandika hotuba ya kushawishi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kuandika hotuba ya kushawishi na kuisambaza kwa mtandao.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika hotuba ya kushawishi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapokubaliana na maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Uraia: mwanafunzi anapoandika hotuba ya kushawishi kuhusu suala lengwa.
- Masuala ya afya: mwanafunzi anapoandika hotuba kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English: somo hili linashughulikia dhana uandishi wa kiuamilifu.
- Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia magonjwa mbalimbali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Kielelezo cha hotuba, tarakilishi/kipakatalishi vyenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.4 Sarufi** | **12.4.1 Aina za Sentensi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya sentensi tata ili kuitofautisha na aina nyingine za sentensi.<br>b) kutambua sentensi tata katika matini.<br>c) kuchambua maana mbalimbali ya sentensi tata.<br>d) kujenga ujuzi wa kuchanganua maana mbalimbali katika sentensi tata ili kufasiri habari kikamilifu. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutoa maelezo ya sentensi tata kwa usahihi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua sentensi tata kwenye orodha ya sentensi kwenye vitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua sentensi tata kwenye orodha ya sentensi kwenye vitabu, chati zilizo na maandishi ya breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua sentensi tata zinazojitokeza katika vifungu akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutolea wenzake maana tofauti za sentensi tata alizozitambua.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi tata kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha.<br>● Mwanafunzi awasilishe darasani sentensi tata alizozitunga ili wenzake wazitolee maoni kwa heshima na upendo. | Mbona tunatambua sentensi tata katika matini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi amtungie mzazi au mlezi wake sentensi tata zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutambua sentensi tata.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi tata ipasavyo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua sentensi tata katika kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtungia mzazi au mlezi wake sentensi tata zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English: masomo haya pia yanashughulikia aina za sentensi.
- Agriculture and Nutrition: masomo haya pia yanashughulikia magonjwa mbalimbali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi, chati, vitabu vilivyoidhinishwa

| 13.0 MSHIKAMANO WA KIJAMII | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Llilopendekezwa** |
| **13 .1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **13.1.1 Mazungumzo** Mawaidha<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br><br>a) kueleza maana ya mawaidha ili kuipambanua,<br>b) kufafanua ujumbe na sifa za mawaidha ya kifasihi,<br>c) kueleza vipengele vya uwasilishaji wa mawaidha,<br>d) kutambua washiriki katika mawaidha ya fasihi simulizi,<br>e) kuchambua sifa za washiriki katika mawaidha ya fasihi simulizi,<br>f) kuwasilisha mawaidha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji,<br>g) kufurahia kushiriki katika uchanganuzi wa wahusika katika tungo za fasihi simulizi. | • Mwanafuzi aelekezwe kueleza maana ya mawaidha akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujadili ujumbe wa mawaidha ya kifasihi akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujadili na wenzake sifa za mawaidha ya kifasihi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kueleza vipengele vya uwasilishaji wa mawaidha.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua washiriki *(fanani, hadhira*) katika mawaidha anayoisikiliza.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuchambua sifa za washiriki katika mawaidha anayoisikiliza kutoka kwa vifaa vya kidijitali, mgeni mwalikwa au mwalimu akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutunga mawaidha kuhusu suala lengwa na kuwawasilishia wenzake darasani.<br>• Mwanafunzi asikilize mawaidha atakayotolewa na mzazi au mlezi wake. | Kwa nini ni muhimu kutoa Mawaidha? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu wahusika katika mawaidha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikilizia mawaidha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapowatolea wenzake mawaidha.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochanganua washiriki katika mawaidha.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowatolea wanafunzi mawaidha darasani kwa ukakamavu.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki mawaidha kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English: Somo hili pia linashughulikia tungo za fasihi simulizi.
- Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia mshikamano wa jamii mbalimbali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi)

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.2 Kusoma** | **13.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>Ushairi<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mbinu za lugha katika fasihi,<br>b) kuchanganua matumizi ya lugha katika mashairi,<br>c) kutumia mbinu mbalimbali za lugha katika mashairi,<br>d) kuchambua shairi kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za lugha,<br>e) kuchangamkia matumizi ya lugha katika ushairi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua mbinu za lugha akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili mbinu za lugha kwa mujibu wa mashairi aliyosoma akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga shairi jepesi (lisilozidi beti tatu) kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za lugha akishirikiana na wenzake na kuliwasilisha darasani.<br>● Mwanafunzi aelekezwe ahakiki uwasilishaji wa wenzake kuhusu matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha katika mashairi waliyotunga na kuyatolea maoni.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuchambua shairi kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za lugha akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kufanya utafiti mtandaoni kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuhusu matumizi ya lugha katika mashairi na kumweleza mzazi, mlezi au mwenzake. | Kwa nini tunatumia mbinu za lugha katika shairi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kutambua mbinu za lugha kwenye mashairi aliyosoma.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga shairi jepesi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapowasilishia wenzake shairi jepesi alilotunga akizingatia mbinu mbalimbali za lugha.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti maktabani na mtandaoni kwa kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuhusu matumizi ya mbinu za lugha katika mashairi. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili matumizi ya mbinu za lugha katika mashairi huku akithamini maoni yao.<br>● Upendo: mwanafunzi anapohakiki uwasilishaji wa wenzake wa mashairi huku akiwakosoa kwa upendo na kuwahimiza.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojukumika kujiandaa ipasavyo ili kuwasilishia wenzake shairi alilotunga.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kutambua mbinu mbalimbali za lugha. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Masuala ya kijamii: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English: masomo haya pia yanashughulikia kusoma kwa kina.<br>● Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia mshikamano wa jamii mbalimbali. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi,  vitabu vyenye maandishi ya breli, vitabu vyenye hati zinazofaa, nakala za mashairi, |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.3 Kuandika** | **13.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>Maelezo<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya insha ya maelezo kuhusu hali<br>b) kutambua vipengele vya insha ya maelezo kuhusu hali<br>c) kuandika insha ya maelezo kuhusu hali akizingatia vipengele vyake<br>d) kufurahia kutunga insha za maelezo kuhusu hali. | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadili dhana ya insha ya maelezo kuhusu hali akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya insha ya maelezo kuhusu hali.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya insha ya maelezo kuhusu hali katika kielelezo cha insha akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo inayohusu hali kutumia tarakilishi *yenye teknoljia saidizi* akizingatia vipengele vyake.<br>● Mwanafunzi amsomee au kumtumie mwenzake insha ya maelezo inayohusu hali kupitia mtandao ili kuitathmini.<br>● Mwanafunzi amsomea mzazi au mlezi wake insha ya maelezo kuhusu hali aliyoandika ili atoe maoni. | Je, kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele katika kuandika insha ya maelezo kuhusu hali? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu insha ya maelezo kuhusu hali.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kuandika insha ya maelezo na kumtumia mwenzake kwa mtandao.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu hali.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo ya hali kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English: masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa insha za maelezo.
- Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia mshikamano wa jamii mbalimbali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Kielelezo cha insha ya maelezo, tarakilishi/kipakatalishi chenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.4 Sarufi** | **13.4.1 Ukanushaji**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanushaji wa hali ya masharti **-nge-, -ngali**, na **-ki-** katika matini,<br>b) kutumia hali ya ukanushaji wa hali ya masharti ya **-nge, -ngali** na **-ki-** ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi sahihi ya ukanushaji wa hali ya masharti ya **-nge**, **-ngali-** na **-ki-** katika maisha ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua ukanushaji wa sentensi katika hali ya masharti ya **-nge-**, **-ngali-** na **-ki-** katika matini mbalimbali *yenye fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza (k.v. orodha ya sentensi, chati).* Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua ukanushaji wa sentensi katika hali ya masharti ya **-nge-**, **-ngali-** na **-ki-** katika matini mbalimbali yenye maandishi ya breli (k.v. orodha ya sentensi, chati yenye maandishi ya breli).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kukanusha sentensi katika hali ya masharti ya **-nge-, -ngali** na **-ki-** katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi zinazoonyesha ukanushaji wa sentensi katika hali ya masharti ya **-nge, -ngali-** na **-ki-** akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia ukanushaji wa masharti ya **-nge-, -ngali-** na **-ki** kuandika kifungu kifupi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi amweleze mzazi, mlezi au mwezake namna ya kukanusha hali ya | Unakanusha vipi sentensi kutumia hali ya masharti? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | masharti ya **-nge-, -ngali-** na **-ki-** zinavyokanushwa. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu mada lengwa na kuwasambazia wenzake wazitolee maoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha ukanushaji wa hali ya masharti.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua ukanushaji wa hali ya masharti na kuutungia sentensi sahihi.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**
Masuala ya mshikamano wa kijamii: wanapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English: somo hili linashughulikia ukanushaji.
- Social Studies na Religious Education: masomo haya pia yanashughulikia mshikamano wa jamii mbalimbali.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**
Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, orodha ya sentensi, chati, vifaa vya breli

| **14.0 MATUMIZI YA USHURU** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **14.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **14.1.1 Mawaidha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya lugha vinavyotumika katika mawaidha,<br>b) kueleza umuhimu wa vipengele vya lugha vinavyotumika katika mawaidha,<br>c) kueleza ishara zifaazo katika kutoa mawaidha,<br>d) kutoa mawaidha kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya lugha ya mawaidha na ishara zifaazo,<br>e) kuonea fahari utoaji wa mawaidha katika maisha ya kila siku. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya lugha kwa kusikiliza mawaidha yakitolewa na mwalimu, mwanafunzi mwenzake, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili umuhimu wa vipengele vya lugha vilivyotumika katika mawaidha aliyosikiliza akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ajadili ishara zifaazo katika kutoa mawaidha, mwanafunzi asiyeona ajadili toni/kiimbo kifaacho katika kutoa mawaidha.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutoa mawaidha kwa mwenzake yanayohusiana na matumizi ya ushuru akizingatia vipengele mbalimbali vya lugha.<br>● Mwanafunzi asikilize mawaidha yakitolewa na mzazi au mlezi wake na kutambua vipengele vya lugha katika mawaidha hayo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusakura mtandaoni akutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kusikiliza mawaidha mbalimbali kisha atambue vipengele vya lugha katika mawaidha hayo | Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele mbalimbai unapotoa mawaidha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kumweleza mzazi, mlezi au mwenzake vipengele vya lugha ya mawaidha. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu vipengele vya lugha vilivyotumika katika mawaidha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika kusikiliza mawaidha yakitolewa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapomtolea mwenzake mawaidha.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutambua vipengele vya lugha katika mawaidha. Pia anapotolea wenzake mawaidha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kusikiliza mawaidha yakitolewa mtandaoni na kutambua vipengele vya lugha vilivyotumika.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

Ujuzi wa matumizi ya fedha: mwanafunzi anapotoa mawaidha yanayohusiana na matumizi ya pesa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English, Indigenous Languages na Foreign Languages: masomo haya pia yanashughulikia mawaidha kama tungo za fasihi simulizi.
- Business Studies: somo hili pia linashughulikia ujuzi wa matumizi ya fedha.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

Mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.2 Kusoma** | **14.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha mjadala,<br>b) kueleza maana ya msamiati na vifungu kama vilivyotumiwa katika kifungu cha mjadala,<br>c) kuchanganua mitazamo katika kifungu cha mjadala,<br>d) kufurahia kusoma kwa ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | ● Mwanafunzi aelekezwe kudondoa habari mahususi kwa mujibu wa kifungu cha mjadala alichokisoma akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusakura mtandaoni kifungu cha mjadala kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, akisome na kudondoa habari mahususi katika kifungu hicho akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na wenzake maana ya msamiati na vifungu kama vilivyotumiwa katika kifungu cha mjadala.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuchanganua mtazamo katika kifungu cha mjadala akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi amweleze mzazi, mlezi au mwenzake jinsi ya kupata habari mahususi katika kifungu cha mjadala ili watoe maoni. | Utadondoa vipi mambo mhimu katika kifungu cha ufahamu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu kifungu cha mjadala.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusakura mtandao kupata kifungu cha mjadala.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kudondoa habari katika kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma na kudondoa habari kutokana na kifungu cha mjadala.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapodondoa habari katika kifungu.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za pamoja na wengine.

**Masuala Mtambuko**
Ujuzi wa matumizi ya fedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- English: somo hili pia yanashughulikia kusoma kwa ufahamu.
- Pre-technical Studies: somo hili pia linashughulikia ujuzi wa matumizi ya fedha.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**

Vifaa vya kidijitali venye teknolojia saidizi kama vile tarakilishi/vipakatalishi, rununu, projekta , vitabu vyenye maandishi ya breli, vitabu vyenye hati zinazofaa, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.3 Kuandika** | **14.3.1 Insha za Kiuamilifu**<br><br>Shajara<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza umuhimu wa shajara,<br>b) kueleza aina za shajara ili kuzibainisha<br>c) kuandika aina za shajara akizingatia vipengele vyake,<br>d) kuandika aina za shajara akizingatia vipengele vyake na matumizi ya breli ipasavyo,<br>e) kuonea fahari matumizi ya shajara katika maisha ya kila siku. | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadili umuhimu wa shajara akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutafiti maktabani au mtandaoni, akitumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saaidizi, aina za shajara.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili aina za shajara alizozitafiti akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza vipengele vya shajara.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aandike aina za shajara akizingatia vipengele vyake, *Mwanafunzi asiyeona aandike* aina za shajara akizingatia vipengele vyake, matumizi ya mikato, alama za uakifishaji na herufi kubwa za breli.<br>● Mwanafunzi awasomee wenzake shajara aliyoandika ili waitolee maoni. | Kwa nini unazingatia vipengele mbalimbali unapoandika shajara? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili umuhimu wa shajara .<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura na kusoma mtandaoni mifano ya shajara kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi .<br>● Hamu ya ujifunzaji**:** mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika mijadala kundini. |
| **Maadili**<br>● Uaminifu: mwanafunzi anapoandika matukio ya kweli katika shajara.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu na kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini na kuheshimu maoni ya wenzake kundini. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Masuala mtambuko mbalimbali kutokana na masuala yatakayoshughulikiwa na mwanafunzi katika shajara yake. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English na Kenya Sign Language: masomo haya pia yanashughulikia uandishi wa shajara.<br>● Pre-technical Studies: somo hili pia linashughulikia ujuzi wa matumizi ya pesa. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Kielelezo cha insha ya kiuamilifu, shajara, tarakilishi/kipakatalishi chenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.4 Sarufi** | **14.4.1 Udogo na Ukubwa wa Nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua hali ya udogo na ukubwa katika nomino,<br>b) kutumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia kwa ufasaha nomino katika hali ya udogo na ukubwa ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuchopoa nomino katika hali ya udogo na ukubwa kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa na mwenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuorodhesha na kuandika nomino katika hali ya udogo na ukubwa kwenye karatasi ya breli,kadi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua viambishi vya udogo na ukubwa katika maneno akishirikiana na wenzake,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika majina ya vifaa vya darasani katika udogo na ukubwa.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuambatanisha nomino za hali ya wastani na za hali ya udogo na ukubwa kwa usahihi kwenye chati za maneno akishirikiana na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuambatanisha nomino za hali ya udogo na ukubwa kwa usahihi kwenye karatasi za breli au tarakilishi yenye teknolojia saidizi akishirikiana na mwenzake,<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kujaza nafasi katika sentensi kwa kutumia nomino katika hali ya udogo au ukubwa. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika majibu kwa kutumia nomino katika hali ya udogo au ukubwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la matumizi ya ushuru akishirikiana na wenzake. | Utabadilisha vipi nomino katika hali ya ukubwa na udogo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi amtajie mzazi au mlezi wake majina ya vifaa vya nyumbani katika udogo na ukubwa katika, mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutambua nomino katika hali ya udogo na ukubwa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino katika hali ya udogo na ukubwa na kuzitungia sentensi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake nomino katika hali ya udogo na udogo katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Ujuzi wa matumizi ya fedha: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino katika hali ya udogo na ukubwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- English na Kenya Sign Language: masomo haya pia yanashughulikia udogo na ukubwa wa nomino.
- Pre-technical Studies: somo hili pia linashughulikia ujuzi wa matumizi ya pesa.

| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia:**<br>Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi, rununu yenye teknolojia saidizi, chati, kadi maneno, kadi za breli, kapu maneno, vifaa vya breli |
|---|

## 15.0 MAADILI YA KITAIFA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **15.1.1 Kusikiliza kwa Kutathmini**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini,<br>b) kueleza vipengele vya kuzingatia katika kutathmini mazungumzo,<br>c) kusikiliza mazungumzo na kuyatathmini kwa kuzingatia vipengele,<br>d) kuchangamkia kutathmini mazungumzo ili kuimarisha mawasiliano. | • Mwanafunzi aelekezwe kueleza maana ya kusikiliza kwa kutathmini akishirikiana na mwenzake.<br>• Mwanafunzi ajadili vipengele vya kuzingatia katika kutathmini mazungumzo kutoka kwenye mazungumzo mafupi, akishirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi asikilize mazungumzo kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi na kuyatathmini kwa kuzingatia vipengele mbalimbali akishirikiana na wenzake.<br>• Mwanafunzi ashiriki na mzazi au mlezi wake katika mazungumzo kuhusu suala lengwa na kutoa maoni kuhusu suala linalozungumziwa. | 1. Kwa nini unasikiliza kwa kutathmini mazungumzo?<br>2. Utatathminije ufaafu wa mazungumzo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika kujadili kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa kutathmini.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikilizia mazungumzo kuhusu suala lengwa na kutathmini.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotathmini yaliyozungumziwa na kutoa uamuzi kuhusu vipengele ambavyo vimetumiwa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofanikiwa kutoa mtazamo wake kuhusu suala linalozungumziwa katika mazungumzo aliyoyasikiliza.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo kuhusu suala lengwa na mzazi au mlezi wake na kujifunza zaidi vipengele vya kusikiliza kwa kutathmini. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoyathamini maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anaposhirikiana wenzake katika mazungumzo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● English: masomo haya pia yanashughulikia aina za usikilizaji. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Mgeni mwalikwa, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta), mti maneno, kapu maneno, vitabu mbalimbali vyenye hati zinazofaa, vitabu vyenye maandishi ya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.2 Kusoma** | **15.2.1 Ufupisho**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza vipengele vya kuzingatia katika ufupisho wa habari katika matini,<br>b) kuandika ufupisho wa habari kwa kuzingatia vipengele vifaavyo,<br>c) kuandika ufupisho wa habari kwa kuzingatia vipengele vifaavyo, sheria za matumizi ya mikato, alama za uafikishaji na herufi kubwa za breli (*mwanafunzi asiyeona*),<br>d) kufurahia kufupisha habari kwa usahihi katika miktadha mbalimbali. | ● Mwanafunzi ajadili vipengele vya ufupisho wa habari katika matini *(kuzingatia maelekezo ya ufupisho, kueleza habari upya kwa maneno yake mwenyewe, kudondosha mifano na maelezo ya ziada, mpangilio wenye muwala)* akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika ufupisho wa habari kwa kuzingatia vipengele vifaavyo na kuwasomea wenzake ili watoe maoni yao. Mwanafunzi asiyeona andike ufupisho wa habari kwa kuzingatia vipengele vifaavyo kama vile sheria za matumizi ya mikato, alama za uafikishaji na herufi kubwa za breli na kuwasomea wenzake ili watoe maoni yao.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma matini mbalimbali zenye fonti zinazofaa zikiwemo za mtandaoni na kufupisha habari kwa usahihi. Mwanafunzi asiyeona asome matini mbalimbali zenye maandishi ya breli zikiwemo za mtandaoni na kufupisha habari kwa usahihi.<br>● Mwanafunzi amsome mzazi, mlezi au mwenzake habari aliyoifupisha kutoka katika matini aliyoisoma ili aitolee maoni. | Kwa nini ni muhimu kuzingatia vipengele mbalimbali ili kuandika ufupisho ufaao? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia katika ufupisho wa habari.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali *vyenye teknolojia saidizi*
- katika kusoma makala.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoeleza kwa kifupi makala aliyosoma.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma makala kutoka mtandaoni na kuyafupisha ipasavyo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anaposoma na kufupisha habari katika matini kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- English: somo hili pia linashughulikia dhana ya ufupisho.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia:**
Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, vitabu vyenye maandishi ya breli na vitabu vyenye hati zinazofaa, vifaa vya breli

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.3 Kuandika** | **15.3.1 Kujibu**<br><br>**(**Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza vipengele vya kuzingatia katika kujibu baruapepe<br>b) kujibu baruapepe kwa kuzingatia vipengele vifaavyo<br>*c) kujibu baruapepe kwa kuzingatia vipengele na matumizi ya breli yafaayo.*<br>d) kujenga mazoea ya kujibu baruapepe ipasavyo. | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadili vipengele vya kuzingatia katika kujibu baruapepe akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua na atumie lugha inayofaa kwa uandishi wa barua ya kujibu baruapepe.<br>● Mwanafunzi ajadili vidokezo vya kutumia katika kujibu baruapepe akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika baruapepe kuhusu suala lengwa kwenye tarakilishi yenye teknolojia saidizi na kuwasambazia wenzake kupitia mtandao.<br>● Mwanafunzi amweleze mzazi au mlezi namna ya kujibu baruapepe ili watoe maoni. | 1. Je, mbona ni muhimu kuzingatia vipengelevipengele mbalimbali unapoandika baruapepe?<br>2. Je, utajibu vipi baruapepe ukuzingatia mambo yafuatayo? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kujibu baruapepe.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kuandika baruapepe na kuisambazia wenzake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika baruapepe ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji**:** mwanafunzi anapomwelezea mzazi au mlezi wake namna ya kujibu baruapepe.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anapoandika baruapepe kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● English: masomo haya pia yanashughulikia kujibu baruapepe.<br>● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia:**<br>Kielelezo cha baruapepe, tarakilishi/kipakatalish chenye teknolojia saidizi, vifaa vya breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzanji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.4 Sarufi** | **15.4.1 Usemi Halisi** na **Usemi wa Taarifa**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kueleza kanuni za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa,<br>b) kutumia usemi halisi na usemi wa taarifa ipasavyo katika matini, | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na wenzake kanuni za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa.<br>● Mwanafunzi ashiriki kugeuza sentensi zilizo katika usemi halisi ziwe katika usemi wa taarifa akishirikiana na wenzake. | 1. Usemi halisi unatofautianaje na usemi wa taarifa?<br>2. Unaaandika vipi usemi halisi?<br>3. Unaaandika vipi usemi wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | c) kuchangamkia matumizi ya usemi halisi na usemi wa taarifa katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi ashiriki kugeuza sentensi zilizo katika usemi wa taarifa ziwe katika usemi halisi akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi ashiriki katika mchezo wa kuchopoa kadi katika vikundi. Kikundi kimoja kichopoe kadi ya sentensi sahili katika usemi halisi na kikundi kingine kichopoe sentensi hiyo katika usemi wa taarifa. Mwanafunzi asiyeona ashiriki katika zoezi la kuorodhesha sentensi katika vikundi. Kikundi kimoja kiorodheshe sentensi sahili katika usemi halisi na kingine kiorodheshe sentensi katika usemi halisi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutunga sentensi sahili katika usemi halisi na usemi wa taarifa daftarini mwake kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la maadili ya kitaifa, mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutunga sentensi sahili katika usemi halisi na usemi wa taarifa karatasini mwake mwa breli kwa kuzingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la maadili ya kitaifa<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi, mlezi au mwenzake sentensi sahili alizozitunga za usemi halisi na usemi wa taarifa ili kuzitolea maoni. | taarifa? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kujadili kuhusu usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mwenzake sentensi sahili alizotunga za usemi halisi na usemi wa taarifa.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Maadili ya kitaifa: mwanafunzi anapotumia usemi halisi na usemi wa taarifa kuhusu suala lengwa kulingana na sentensi zilizotungwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● English: somo hili pia linashughulikia usemi halisi na usemi wa taarifa.<br>● Social Studies: somo hili pia linashughulikia masuala ya kijamii. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia**<br>Kadi za sentensi, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, Mti maneno, vitabu mbalimbali vyenye hati zinazofaa na vitabu vyenye maandishi ya breli |

## VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINI

| STADI YA KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali Na Matarajio** |
| **Kuweza kuwasiliana kwa njia ifaayo (***matamshi, kiimbo na kusikika na uakifishaji***)** | Anawasiliana kwa njia ifaayo kwa kuzingatia vipengele 4 vya kuwasiliana. | Anawasiliana kwa njia ifaayo kwa kuzingatia vipengele 3 vya kuwasiliana. | Anawasiliana kwa njia ifaayo kwa kuzingatia vipengele 2 vya kuwasiliana. | Anawasiliana kwa njia ifaayo kwa kuzingatia kipengele 1 cha kuwasiliana. |
| **Kuweza kufasiri habari katika suala lengwa** *(majibu sahihi, matumizi ya msamiati mwafaka.*) | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa alilosikiliza kwa kuzingatia vipengele 3 vya kufasiri habari. | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa alilosikiliza kwa kuzingatia vipengele 2 vya kufasiri habari. | Anatoa maelezo sahihi kuhusu suala lengwa alilosikiliza kwa kuzingatia kipengele 1 cha kufasiri habari. | Anatoa maelezo kuhusu suala lengwa alilosikiliza kwa kuzingatia kipengele 1 cha kufasiri habari. |
| **Kuweza kutumia msamiati na istilahi za suala lengwa** *(Msamiati wa heshima, adabu, maamkuzi, maagano visawe, methali, tashbihi)* | Anatumia msamiati na istilahi 6 kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. | Anatumia msamiati na istilahi 4-5 kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. | Anatumia msamiati na istilahi 2-3 kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. | Anatumia msamiati na istilahi 1 kujieleza kulingana na muktadha/suala lengwa. |
| **Kuweza kutumia ishara za mwili ipasavyo** (*jinsi anavyoketi au kusimama, ishara za uso, kumtazama msikilizaji kwa ukakamavu)(mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona)* | Anaweza kutumia ishara 4 za mwili ipasavyo anaposikiliza na kuzungumza. | Anaweza kutumia ishara 3 za mwili ipasavyo anaposikiliza na kuzungumza. | Anaweza kutumia ishara 2 za mwili ipasavyo anaposikiliza na kuzungumza. | Anaweza kutumia ishara 1 ya mwili ipasavyo anaposikiliza na kuzungumza. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutumia ishara za mwili ipasavyo** (*jinsi anavyoketi/kusimama, ishara uso, kumsikiliza mwalimu kwa makini,ukakamavu)(mwanafunzi asiyeona)* | Anatumia ishara 4 za uso na mwili ipasavyo kama vile kuketi, kusikiliza mwalimu kwa makini, kuonyesha ukakamavu na kuinua mkono wakati wa kujibu swali. | Anatumia ishara 3 za uso na mwili ipasavyo kama vile kuketi, kusikiliza mwalimu kwa makini na kuonyesha ukakamavu. | Anatumia ishara 2 za uso na mwili ipasavyo kama vile kuketi na kusikiliza mwalimu kwa makini. | Anatumia ishara 1 ya uso na mwili ipasavyo. kama vile kusikiliza mwalimu kwa makini. |
| **Kuweza kuwasilisha utanzu lengwa wa fasihi simulizi** *(semi, ushairi n.k)* | Anawasilisha utanzu lengwa wa fasihi simulizi kwa kwa kuzingatia sifa 6 zinazoubainisha utanzu. | Anawasilisha utanzu lengwa wa fasihi simulizi kwa utendeti kwa kuzingatia sifa kati ya 4-5 zinazobainisha utanzu. | Anawasilisha utanzu lengwa wa fasihi simulizi kwa utendeti kwa kuzingatia sifa kati ya 2-3 zinazoubainisha utanzu. | Anawasilisha utanzu lengwa wa fasihi simulizi kwa utendeti kwa kuzingatia sifa 1 inayoubainisha utanzu. |

| STADI YA KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Vigezo / Viwango** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali Na Matarajio** |
| **Kuweza kufahamu suala lengwa** *(Majibu sahihi, matumizi ya msamiati mwafaka, sababu za suala lengwa k.m kushawishi*) | Anatoa majibu sahihi kwa maswali 5 aliyoulizwa kwenye muktadha. | Anatoa majibu sahihi kwa maswali 3-4 aliyoulizwa kulingana na muktadha. | Anatoa majibu sahihi kwa maswali 2 aliyoulizwa kulingana na muktadha. | Anatoa jibu sahihi kwa maswali 1 aliyoulizwa kulingana na muktadha. |
| **Kuweza kusoma kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki wa fasihi kwa ufasaha. (***Maudhui, dhamira, wahusika, ploti, wahusika n.k)* | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 5 vya uhakiki wa fasihi kwa ufasaha na urahisi. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 4 vya uhakiki wa fasihi kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele kati ya 2-3 vya uhakiki wa fasihi. | Anajaribu kusoma kwa kuzingatia kipengele 1 cha uhakiki wa fasihi. |
| **Kuweza kufupisha ujumbe kwenye matini aliyoisoma** | Anafupisha ujumbe kwenye matini aliyoisoma kwa hoja 7 kuu. | Anafupisha ujumbe kwenye matini aliyoisoma kwa hoja kati ya 5-6 kuu. | Anafupisha ujumbe kwenye matini aliyoisoma kwa hoja kati ya 3-4 kuu. | Anafupisha ujumbe kwenye matini aliyoisoma kwa hoja 1-2 kuu. |
| **Kasi ya usomaji** (*Idadi ya maneno yanayosomwa kwa usahihi kwa muda wa dakika moja*) | Anasoma kwa usahihi zaidi ya maneno **75** kwa muda wa dakika moja. | Anasoma kwa usahihi maneno **50-74** kwa muda wa dakika moja. | Anasoma kwa usahihi kati ya maneno **20-49** kwa muda wa dakika moja | Anasoma kwa usahihi kati ya maneno 1-19 kwa muda wa dakika moja. |

| STADI YA KUANDIKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Vigezo / Viwango** | **Kuzidisha matarajio** | **Kufikia matarajio** | **Kukaribia matarajio** | **Mbali na matarajio** |
| Kuweza kuzingatia sarufi na ufundi wa uandishi | Anaandika insha kwa kuzingatia alama za uakifishaji. Anadhihirisha umilisi wa kiwango cha juu cha sarufi na uendelezaji wa maneno katika uandishi wake uko sawa. | Anaandika insha kwa kuzingatia alama za uakifishaji na kuendeleza maneno ipasavyo katika uandishi. Hata hivyo, ana makosa machache ambayo hayatatizi usomaji. | Anaandika insha kwa kuzingatia baadhi ya alama za uakifishaji na maendelezo ya maneno ambayo yanatatiza usomaji wa sehemu za insha yake. | Anaandika insha kwa kuzingatia baadhi ya alama za uakifishaji na maendelezo ya maneno katika insha yake yanadhihirisha makosa ya kisarufi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa uandishi.<br>Msomaji anaweza tu kukisia maana. |
| Kuweza kuandika kwa kuzingatia mada lengwa | Anaandika insha kwa ubunifu na lugha komavu kwa kuzingatia mada aliyopewa. | Anaandika insha kwa ubunifu kwa kuzingatia mada aliyopewa. | Anaandika insha kwa kuzingatia mada aliyopewa. | Anaandika insha bila kuzingatia mada aliyopewa. |
| Kuweza kuandika kwa hati nzuri | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br>Anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno kutoka mwanzo hadi mwisho wa | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br>Anatenganisha herufi nyingi ipasavyo. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno. | Ana mwandiko usio nadhifu lakini unasomeka.<br>Anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo. Anaacha nafasi zisizolingana baina ya | Ana mwandiko usiosomeka kwa urahisi.<br>Hatenganishi herufi nyingi ipasavyo. Anaacha nafasi nyingi zisizolingana baina ya maneno. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | insha. | | maneno. | |
| Kuweza kutumia msamiati anuwai unaolingana na mada anayoiandikia insha. | Anatumia misamiati 4 anuwai unaolingana na mada anayoiandikia insha. | Anatumia misamiati 3 anuwai unaolingana na mada anayoiandikia insha. | Anatumia misamiati 2 anuwai unaolingana na mada anayoiandikia insha. | Anatumia msamiati 1 anuwai unaolingana na mada anayoiandikia insha. |
| Kuweza kuzingatia muundo na mtindo wa insha lengwa. | Anaandika kwa kuzingatia muundo na mtindo wa insha 3 na kuziandika kwa ubunifu mkuu. | Anaandika kwa kuzingatia muundo na mtindo wa insha 3. | Anaandika kwa kuzingatia muundo na mtindo wa insha 2. | Anaandika kwa kuzingatia muundo na mtindo wa insha 1. |
| Kuweza kutambua aina za maneno katika matini za Kiswahili | Anatambua aina 8 za maneno katika matini alizopewa kulingana na maagizo. | Anatambua aina za maneno kati ya 6-7 katika matini alizopewa kulingana na maagizo. | Anatambua aina za maneno kati ya 4-5 katika matini alizopewa kulingana na maagizo. | Anatambua aina za maneno kati ya 1-3 katika matini alizopewa kulingana na maagizo. |
| Kuweza kubainisha ngeli za nomino mbalimbali | Anabainisha ngeli 7 za nomino alizopewa kwa usahihi. | Anabainisha ngeli 5-6 za nomino alizopewa kwa usahihi. | Anabainisha ngeli za nomino kati ya 3-4 alizopewa kwa usahihi. | Anabainisha ngeli za nomino kati ya 1-2 alizopewa kwa usahihi. |
| Kuweza kutunga sentensi za aina mbalimbali kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi | Anatunga sentensi 3 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao kwa maelezo. | Anatunga sentensi 3 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao. | Anatunga sentensi 2 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao. | Anatunga sentensi 1 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao |

| STADI YA SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali Na Matarajio** |
| Kuweza kutambua aina za maneno katika matini za Kiswahili | Anatambua aina 8 za maneno katika matini alizopewa kulingana na maagizo. | Anatambua aina za maneno kati ya 6-7 katika matini alizopewa kulingana na maagizo. | Anatambua aina za maneno kati ya 4-5 katika matini alizopewa kulingana na maagizo. | Anatambua aina za maneno kati ya 1-3 katika matini alizopewa kulingana na maagizo. |
| Kuweza kubainisha ngeli za nomino mbalimbali | Anabainisha ngeli 7 za nomino alizopewa kwa usahihi. | Anabainisha ngeli 5-6 za nomino alizopewa kwa usahihi. | Anabainisha ngeli za nomino kati ya 3-4 alizopewa kwa usahihi. | Anabainisha ngeli za nomino kati ya 1-2 alizopewa kwa usahihi. |
| Kuweza kutunga sentensi za aina mbalimbali kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi | Anatunga sentensi 3 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao kwa maelezo. | Anatunga sentensi 3 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao. | Anatunga sentensi 2 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao. | Anatunga sentensi 1 sahihi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi ufaao |
| Kuweza kunyambua vitenzi vya Kiswahili ipasavyo | Ananyambua vitenzi 4 katika sentensi au matini kwa kuzingatia kauli aliyopewa. | Ananyambua vitenzi 3 katika sentensi au matini kwa kuzingatia kauli aliyopewa. | Ananyambua vitenzi 2 katika sentensi au matini kwa kuzingatia kauli aliyopewa. | Ananyambua kitenzi 1 katika sentensi au matini kwa kuzingatia kauli aliyopewa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kutumia lugha kwa usahihi *(uakifishaji, ukanushaji, umoja, wingi, udogo, ukubwa, kuandika vinyume n.k)* | Anazingatia kanuni 6 za lugha ipasavyo katika matini utendeti. | Anazingatia kanuni 4-5 za lugha ipasavyo katika matini. | Anazingatia kanuni 2-3 za lugha ipasavyo katika matini. | Anazingatia kanuni 1 ya lugha ipasavyo katika matini. |

## KIAMBATISHO 1: MWONGOZO WA MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI KATIKA GREDI YA TISA

### UTANGULIZI

Katika Gredi ya 9, wanafunzi watashiriki katika Mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji kwa kuchagua kutoka somo moja au kwa kuunganisha masomo mbalimbali. Mradi wa CSL utamwezesha mwanafunzi aliye na changamoto za kuona kutumia maarifa na ujuzi kutoka masomo mengine kushughulikia tatizo katika jamii. Utekelezaji wa mradi huu wa CSL utachukua Mtazamo Kamili wa Shule, ambapo wanachama wote wa jamii ya shule ikiwa ni pamoja na walimu, utawala wa shule, wazazi/walezi/ jamii na wafanyakazi wengine wa shuleni. Itakuwa jitihada za ushirikiano ambapo mwalimu wa Somo la Kijamii (Social Studies) anaratibu na kufanya kazi na walimu wengine wa masomo mbalimbali kubuni na kutekeleza miradi ya CSL pamoja. Walimu watachagua mada kutoka kwa masomo mbalimbali na mada tofauti tofauti za masuala mtambuko (PCIs) kwa mradi wa CSL. Pia inapaswa kutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili. Wanafunzi watashiriki katika mradi mmoja wa pamoja wa darasa wa CSL uliounganishwa ukifuata hatua 6 za maendeleo kama ifuatavyo:

| Hatua | Maelezo |
|---|---|
| **Hatua ya 1** | **Utambuzi wa Tatizo**<br>Wanafunzi wanachunguza jamii yao ili kuelewa changamoto zinazokabiliwa na athari zake kwa wanajamii. Baadhi ya changamoto katika jamii zinaweza kuwa:<br>● Uharibifu wa mazingira<br>● Magonjwa ya mienendo ya maisha, magonjwa ambukizi na yasiyoambukizwa<br>● Umaskini<br>● Misukosukona migogoro katika jamii<br>● Uhifadhi wa vyakula |
| **Hatua 2** | **Kubuni Suluhisho**<br>Wanafunzi wanabuni njia ya kuingilia kati kushughulikia changamoto iliyotambuliwa. |
| **Hatua 3** | **Mpango wa Mradi**<br>Wanafunzi wanagawana majukumu, kutengeneza orodha ya shughuli zitakazofanywa, kuandaa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kutekeleza mradi, na kuweka ratiba za utekelezaji. |
| **Hatua 4** | **Utekelezaji**<br>Wanafunzi wanatekeleza mradi na kuweka idhibati wa kazi iliyofanywa. |

| | |
|---|---|
| **Hatua 5** | **Kuonyesha Mradi na Kuandika Ripoti**<br><br>Maonyesho ni pamoja na kuonyesha vitu vya mradi wa wanafunzi kwa jamii na kutafakari kuhusu maoni wanayopokea.<br><br>Wanafunzi wanandika ripoti inayoelezea shughuli za mradi wao na mafunzo waliyopata kutokana na maoni waliyopewa. |
| **Hatua 6** | Tafakuri<br>Wanafunzi wanapitia kazi yote ya mradi kujifunza kutokana na changamoto walizokutana nazo. Wanahusisha kazi ya mradi na dhana za masomo, wakiangazia jinsi dhana hizo ziliwasaidia kutekeleza mradi pamoja na jinsi mradi ulivyosaidia kuimarisha uelewa wao wa dhana za masomo. |

**TANBIHI**: Hatua hizi zitapangwa kwa muda katika mihula mitatu ya kalenda ya masomo.

**Tathmini ya miradi ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji (CSL)**

Tathmini kwa ajili ya mradi wa CSL uliounganishwa utafanywa kwa njia ya tathmini ya mara kwa mara. Tathmini itazingatia mchakato na matokeo ya mwisho. Hii inajumuisha kutathmini kila hatua ya maendeleo ya mradi wa darasa wa CSL. Itatazama vipengele vitatu, yaani: ujuzi kutoka masomo mbalimbali uliotumika katika kutekeleza mradi, umilisi wa kimsingi uliokuzwa, na maadili yaliyokuzwa.

**KIAMBATISHO 2: MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

| Mada | Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| **Kusikiliza na Kuzungumza** | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi kufanyiana tathmini | ● Chati/chati za breli<br>● Michoro na picha/maelezo ya michoro na picha<br>● Mgeni mwalikwa<br>● Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>● Mti maneno<br>● Kapu maneno/ orodha maneno<br>● Vitabu mbalimbali vya breli/vyenye fonti zifaazo | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |
| **Kusoma** | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa | ● Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi<br>● Kinasasauti chenye teknolojia saidizi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | • Rununu yenye teknolojia saidizi | |
| | b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kusoma kwa sauti<br>e) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>f) Potifolio<br>g) Shajara | • Projekta<br>• Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi<br>• Kinasasauti chenye teknolojia saidizi<br>• Rununu yenye teknolojia saidizi<br>• Kamusi mbalimbali | 3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |
| **Kuandika** | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potifolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | • Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Kielelezo cha insha ya wasifu<br>• Nakala ya barua ya kirafiki<br>• Nakala ya barua rasmi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Sarufi** | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza mapengo<br>d) Kutunga sentensi<br>e) Kazi mradi | • Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi<br>• Kinasasauti chenye teknolojia saidizi<br>• Rununu yenye teknolojia saidizi<br>• Projekta<br>• Kapu maneno/ orodha maneno<br>• Mti maneno<br>• Kadi maneno/ kadi za breli<br>• Maelezo ya picha/picha za vitu mbalimbali<br>• Michoro/ maelezo ya michoro<br>• Chati/chati za breli<br>• Nyenzo halisi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |